# Nipashe Jumapili

MWANGA WA JAMII

Jumapili Juni 16, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581709

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




UKURASA 2

**Mwandishi** akamatwa kisa kupiga picha gari la mafuta



UKURASA 2

**Balozi** afariki dunia, kuzikwa kesho



UKURASA 7

**Wadau** wapongeza serikali kudhibiti kupaa bei ya sukari



**Shakira jimbo liko wazi** UK. 20

# Rais Samia akerwa na ubabe ma-RC, ma-DC

• **Asema** baadhi wanajiona miungu watu, afurahia mabadiliko utoaji haki... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea Taarifa ya Kamati ya Kuunda Mkakati wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai kutoka kwa Makamu Mwenyekiti wa Tume hiyo, Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu, Balozi Ombeni Sefue, katika hafla iliyofanyika Ikulu, Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## RIPOTI MAALUM -2

## Karata somo la Uraia likifutwa shule za msingi na sekondari UK. 4

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

### UWEKEZAJI GESI ASILIA, MAFUTA WAPAA



NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amezindua taarifa za utendaji katika sekta ndogo za umeme, gesi asilia na mafuta kwa mwaka 2022/ na kutoa maelekezo mahsusi..

UKURASA WA 17

### RAIS RAMAPHOSA ATAKA SERIKALI MPYA

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, amekuwa katika mtihani wa kutimiza matakwa ya raia wake baada ya kuchaguliwa na bunge kuendelea na nafasi yake kwa awamu ya pili...

## Mangariba wabuni mbinu mpya ukeketaji

UKURASA 3

**MICHEZO** **YANGA KUPIGA KAMBI ULAYA** UK.24

**MAONI,** UK.6

# Balozi Ruhinda afariki dunia

**Na Romana Mallya**

BALOZI wa zamani wa Tanzania katika nchi za Canada na Jamhuri ya Watu wa China na mhariri maarufu wa vyombo vya habari nchini, Ferdinand Ruhinda amefariki dunia.

Taarifa iliyotolewa jana ilieleza kuwa mwanadiplomasia huyo, mwanahabari na mfanyabiashara, alifariki dunia usiku wa kuamkia jana.

Ruhinda ambaye aliwahi kuwa Mhariri Mtendaji wa magazeti ya CCM ya Uhuru na Mzalendo, na yale ya Serikali ya Daily News, Sunday News kwa nyakati tofauti, atazikwa kesho (Jumatatu) katika makaburi ya Kondo, Kunduchi, Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana, amefariki dunia baada ya kuugua kwa muda mrefu maradhi ya kisukari na msiba uko nyumbani kwake Masaki jijini humo. Alikuwa mwanzilishi wa magazeti ya Mwananchi kabla ya kuchukuliwa na kundi la kampuni za Habari la Nation na Radio Uhuru (sasa Uhuru FM).

Balozi Ruhinda ambaye anatoka familia ya uchifu, alipata elimu yake ya uandishi wa habari katika Chuo Kikuu cha Nairobi na kupata mafunzo ya uandishi wa habari ndani na nje ya nchi.

Kabla ya kuingia katika medani ya diplomasia mwanzoni mwa miaka ya 1980, aliwahi kuwa Mhariri Mkuu wa Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD) - sasa TBC Taifa.

Alihudumu ubalozi wa Tanzania nchini Sweden baadaye akateuliwa Balozi wa Tanzania nchini Canada (1983-1988) na China (1989-1992) kabla ya kustaafu.

# Samia akerwa ubabe ma-RC, ma-DC

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan (pichani), amesema bado kuna wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya wanaendeleza ubabe akionya kwamba, kuna usugu wa aina fulani ambao unahitaji kushughulikiwa.

Rais Samia aliyasema hayo jana Ikulu jijini Dodoma katika hafla ya kupokea Ripoti ya Kamati ya Kuandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Tume ya Kuangalia Jinai Nchini.

"Matumizi mabaya ya madaraka linatakiwa kuwa jambo la kihistoria. Waraka namba moja uliotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi unaowataka wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya kuzingatia ipasavyo matumizi ya sheria inayowapa mamlaka ya ukamataji uende ukatekelezwe vyema.

"Pamoja na waraka ule ambao umetolewa mwaka jana (2023) bado kuna wakuu wa mikoa wakuu wa wilaya wanaendeleza ubabe kule maeneo waliko.

"Nikimunukuu makamu mwenyekiti wakati ananipa utangulizi anasema, wakati wa kikao chao na wakuu wa wilaya. Mmoja alithubutu kusimama na kusema 'mimi ni mwakilishi wa Rais hapa kwa hiyo lolote lililopo hapa ni la kwangu, hata kama ni mahakama ikiamua sivyo mimi nitatengua',"alisema.

Kutokana na hayo kuendelea, Rais Samia alisema anadhani bado hawajakaa vizuri ama elimu zaidi inahitajika au kuna usugu wa aina fulani unahitaji kushughulikiwa na kuagiza waraka ule uzingatiwe na kufanyiwa kazi vizuri.

"Nilikuwa ninazungumza na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki Jinai, Balozi Ombeni Sefue, ameniambia kuwa wakati wa kukutana na wakuu wa mikoa na wilaya wengi hawakushiriki vikao hivyo, lakini pia hata mawaziri baadhi yao hawakushiriki.

"Sasa ninaombe kamati hii kuhahakikisha makundi haya yote yanafikiwa kwani bila kuwa na uelewa kuhusu jambo hili, hatuwezi kulifanikisha ni lazima kila mtu apate uelewa," aliagiza Rais Samia.

Alisema kutokana na idadi ya washiriki wa vikao vya ufafanuzi wa mkakati kuwa ndogo ipo haja kwa Tume hiyo kurudia tena ili makundi yote kupata uelewa zaidi wa mkakati huo ulioundwa.

Rais Samia alisema bado baadhi ya wakuu wa mikoa na wilaya wanatumia nafasi zao vibaya ikiwamo kukamata na kuwaweka mahabusu wananchi bila kufuata sheria ya utumishi wa umma.

"Ninaishukuru kamati kwa mapendekezo yake ikiwamo hili la mtushi ambaye atafanya kosa kuweka wananchi ndani na mwananchi akilalamika na kubainika kuwa alikamatwa kinyume hilo, litakuwa kosa lake na serikali haitahusika na kitu chochote," alisema.

Awali, akiwasilisha taarifa hiyo, Balozi Sefue, alisema moja kati ya mambo ambayo wameyabaini ni bajeti pungufu kulinganisha na hali halisi kwenye taasisi nyingi za haki jinai nchini katika miaka mitatu ya fedha.

Alisema taasisi hizo ni mahakama, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Jeshi la Polisi, magereza, TAKUKURU na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

"Katika kipindi hicho cha miaka mitatu taasisi hizi zilipokea Sh. trilioni 1.99 sawa na wastani wa Sh. bilioni 662.6 tu kwa mwaka. Shilingi trilioni 1.86 kutoka bajeti ya serikali na Sh. bilioni 127.78 ku-



toka washirika wa maendeleo," alisema.

Alisema kamati imefanya uchambuzi wa mahitaji ya rasilimali fedha ambayo yatahitajika na sehemu kubwa ikiwa na marekebisho ya miundombinu ya majengo na vitendea kazi.

"Hii ni kutoka na hali iliyobainika kuwa kwa miaka mingi sana bajeti iliyokuwa inatolewa kwa taasisi hizi ilikuwa chini sana ya mahitaji halisi.

"Kamati inapendeza uwapo mpango mahsusi wa kuongeza bajeti katika miaka mitano mfululizo ya kutekeleza mkakati huu ili kupunguza kwa kiasi kikubwa upungufu ulipo ikiwamo ujenzi wa majengo na miundombinu mingine," alisema Balozi Sefue.

# Mwandishi akamatwa kisa kupiga picha gari la mafuta

**Na Waandishi Wetu**

NAIBU Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Jamhuri, Manyerere Jackton, amekamatwa na kushikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Kilimanjaro, kwa zaidi ya saa mbili na nusu kwa kupiga picha lori lililopinduka.

Akiwa safarini eneo la mji wa Same, Manyerere alikuta lori lililobeba mafuta ya kula likiwa limepinduka na wananchi wanaokadiriwa kuwa hadi 200 wamelivamia wakiwa na ndoo na madumu yaliyoashiria kuchota mafuta hayo.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Manyerere alisema baada ya kukuta tukio hilo saa 4:00 asubuhi alipiga picha na akiwa katika kufanya hivyo, ghafla polisi wasiozidi saba walimvamia na kuanza kumghasi kisha kuchukua simu aliyokuwa akiitumia kupiga picha na kufuta kila alichorekodi.

"Ilikuwa asubuhi majira ya saa 4:00, nilikuwa nje kidogo ya mji wa Same kama kilomita 15 hivi. Nilifika pale nikaona kuna ajali, nikaegesha gari pembeni nikashuka nikaanza kuzungumza na askari wakasema ni ajali ya semi trailer lililokuwa limebeba mafuta ya kula.

"Ajali ilitokea usiku kwahiyo, wananchi wakaingia pale wakaanza kumpiga dereva na wakaanza kufanya vurugu na kupora mafuta.

"Wamepora (mafuta), polisi walivyofika pale wakaanza kuzuia. Kwa hiyo mimi nilipofika pale nikakuta kundi kubwa la wananchi wako takribani kama 150 au 200 hivi, wako upande wa pili wa barabara wana ndoo na vyombo vya kuteka yale mafuta," anasimulia Manyerere.

Manyarere alisema walipomkamkata, walimpeleka hadi Kituo Kikuu cha Polisi Wilaya ya Same, kwa lengo la kumhoji lakini aliachiwa baadaye kwa amri ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Simon Maigwa.

Alisema msukumo alioupata pale ni kwamba imekuwaje mbona kwenye ajali ndiyo watu wanataka wanufaike badala ya kusaidia.

"Kwa hiyo nikapiga picha wale wananchi wakiwa na madumu yao na pembeni gari likiwa limelala. Nikapiga picha kama nne za wananchi na lile lori. Polisi mmoja akaniuliza kwa nini unapiga picha? Nikamjibu ndugu yangu tuko kazini.

"Akauliza tena wewe nani? nikamwambia mimi mwandishi wa habari na Mhariri wa Gazeti la Jamhuri.

Akauliza tena kwa nini unapiga picha bila kibali? Nikamwambia ninapiga picha tukio la barabarani, lakini kama ingekuwa ni Kituo cha Polisi, sawa!

"Wakanikaba pale, walikuwa kama sita au saba hivi. wakaninyang'anya simu, akaja mkubwa wao ana nyota tatu akaamuru niingizwe kwenye gari lao lakini nikagoma. "Tukaenda kituo cha Same nikaa pale kama saa mbili au tatu hivi wakaniachia baada ya mkuu wa kituo kunisikiliza na kuona si kosa," alisimulia.

**POLISI WAFUNGUKA**

Kamanda Maigwa alisema jeshi hilo lililazimika kutumia nguvu kwa kupiga mabomu ya machozi kuwatawanya zaidi ya wananchi 600 waliokuwa wamevamia lori lililokuwa limebeba mafuta ya kula aina ya 'Korie' lililopata ajali eneo la Njoro.

Alisema tukio hilo lilitokea juzi na lori lenye namba za usajili T 783 CTC aina ya HOWO na trela lake namba T 889 CSK likitokea Dar es Salaam kwenda Arusha, liliacha njia na kupinduka, hivyo kusababisha uharibifu huo.

Kamanda Maigwa alisema askari mmoja alijeruhiwa na kitu butu (jiwe) kichwani na mwananchi aliyekuwa akipinga amri ya kuondolewa eneo hilo.

Wakati huo huo, Mwandishi wa Habari na Mmiliki wa Dima Tv, Dina Maningo, aliyeshikiliwa kwa siku mbili na Jeshi la Polisi mkoani Mwanza, aliachiwa kwa dhamana jana jioni.

Dina alikamatwa Alhamisi wiki hii kwa tuhuma za kutumia nyaraka za siri za Jeshi la Polisi za kesi ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Yahaya Nawanda, anayedaiwa kumlawiti mwanafunzi.

Mwenyekiti wa Chama Cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Mwanza, Edwin Soko, aliiambia Nipashe jana kuwa mwandishi huyo ameachiwa kwa dhamana.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, SACP Wilboard Mutafungwa, alisema wanamshikilia Nawanda kwa tuhuma za kumlawiti binti huyo (21) Juni 2, mwaka huu, usiku katika eneo la baa ya The CASK, viwanja vya jengo la Rock City Mall.

Alisema mahojiano yanaendelea kwa kushirikisha taasisi zingine na wakikamilisha watapeleka Ofisi ya Mashitaka ya Taifa.

Kamanda Mutafungwa alisema mtuhumiwa anashitakiwa na Jamhuri na mlalamikaji ni shahidi katika kesi hiyo, huku akikanusha nyaraka zinazosambaa mitandaoni siyo sehemu ya uchunguzi wao.

Alisema gari linalodaiwa kufanyika kitendo hicho wameshalikamata na wanaendelea na mawasiliano na watu wa mkoa wa Simiyu kwa ajili ya kulipeleka Mwanza. Pia aliwataka wanaosambaza habari hizo bila kujali utu wa binti huyo, watambue wako kinyume na sheria ya kulinda utu wa mtu.

## HABARI KITAIFA

# Mangariba wabadili mbinu ukeketaji

**Na Thobias Mwanakatwe,**

SINGIDA

BAADHI ya mangariba mkoani hapa wameibuka na mbinu mpya ya ukeketaji kwa kuwachukua watoto chini ya umri wa miaka mitano wakidai wanakwenda kuwatibu ugonjwa ujulikanao kama 'lawalawa'.

Vitendo hivyo vya ukeketaji vimekuwa vikipigiwa kelele na serikali na makundi mbalimbali ndani ya jamii kwa kuwa vimekuwa vikiwakatili watoto, hasa mabinti.

Mratibu wa kupinga ukatili kutoka Shirika la Empower Society Transform Lives (ESTL), Ruth Ndagu, aliyasema hayo juzi wakati akitoa elimu kwa wanafunzi katika shule nane za msingi na sekondari zilizoko kata ya Ngimu, wilayani Singida.

Shirika hilo linajishughulisha na kuwezesha jamii na kubadili maisha.

Ndagu alisema wakeketaji hao, maarufu kama mangariba, wanachokifanya hivi sasa ili wasibainike na kuchukuliwa hatua, ni kuwachukua watoto wakidai wanawatibu maradhi kumbe wanakwenda kuwakeketa.

"Ukatili mkubwa umeongezeka kwa watoto chini ya miaka mitano ambapo ukeketaji unafanyika kwa njia tofauti watoto hawafahamu kama wanakeketwa, wazazi na walezi wanaelezwa wanakwenda kutibiwa ugonjwa wa lawalawa ambao kwa kabila la Kinyaturu unajulikana kama madudu,"alisema.

Hawa Hussein, ambaye ni ngariba mstaafu, alisema ukatili huo umekuwa ukifanyika nyakati za usiku baada ya mangariba kukubaliana na wazazi na walezi wa watoto. Alisema kutokana na mbinu wanayotumia ya matibabu imekuwa vigumu kujulikana.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Ngaramtoni, Dotto Kasese, alisema watoto wengi wanaofanyiwa ukeketaji huo ni wa kuanzia umri wa miaka sifuri hadi mitatu.

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, Kasese aliomba serikali kufanya uchunguzi na kuchukua hatua kwa wahusika kwa kuwa vitendo hivyo vimekithiri vijijini na kuchangia kuharibu watoto.

Ofisa Elimu Kata ya Ngimu, Tabu Omari, alishukuru Shirika la ESTL kwa kutoa elimu ya ukeketaji kwa wanafunzi wa shule hizo, ambayo itasaidia watoto kujua madhara yake na kuwa mabalozi wa kuwaelimisha wazazi na walezi.

Utafiti uliofanywa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), miaka mitatu iliyopita, ulibainisha kuwa mikoa inayoongoza kwa ukeketaji nchini kuwa ni Mara, Dodoma na Singida.

Katika mikoa hiyo, wananchi wanaamini ili mtoto wa kike avuke kutoka katika hatua ya kuwa msichana kwenda hatua ya utu uzima ni lazima akeketwe.



# Majaliwa mgeni rasmi Baraza Eid el Haj kesho

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa (pichani), kesho anatarajia kuwa mgeni rasmi kwenye Baraza la Eid kitaifa litakalofanyika katika msikiti wa Mfalme Mohamed V1, Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), Kinondoni, Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa taarifa ya Katibu Mkuu BAKWATA, Alhaj Nuru Mruma, wameomba waislamu kujumuika kwa wingi kushiriki swala hiyo.

"Tunaomba Wasilam kujumika kwa wingi kushiriki swala na Baraza la Eid kuanzia saa 1:00 asubuhi," alisema.

Mruma alisema kwa niaba ya BAKWATA, Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Dk. Abubakar Zubeir anawatakia waislam na wananchi wote maandalizi mema ya sikukuu hiyo.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Karata za somo Uraia likifutwa shule za msingi na sekondari



Dk. Aneth Komba



Gratian Mukoba




Prof. Carolyne Nombo

**Na Francis Kajubi**

KATIKA sehemu ya kwanza ya ripoti hii jana, kulikuwa na ufafanuzi wa kina juu ya uhaba wa walimu nchini, nchi ikiwa na walimu 68 tu wenye sifa wanaofundisha somo Uraia kidato cha kwanza hadi cha nne katika shule za sekondari Tanzania Bara.

Katika toleo la leo, linaangazia uamuzi wa serikali kufuta somo hilo katika shule za msingi na sekondari nchini, wataalamu wakikosoa uamuzi. Sasa endelea...

Wizara ya Elimu, Sayanzi na Teknolojia kupitia maboresho ya mwaka jana ya mtaala na Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, imefuta somo la Uraia na kuleta somo jipya linaloitwa Historia ya Tanzania na Maadili.

Wadau wa elimu wametilia shaka uamuzi huo wa serikali wa kulifuta somo la Uraia na badala yake kuleta somo jipya ilhali hakuna walimu wa kutosha waliosomea kufundisha somo hilo katika shule za msingi na sekondari.

Vilevile, wadau hao wanadai kufuta somo la Uraia na kuanzisha somo jipya la Historia ya Tanzania na Maadili kutarudisha nyuma juhudi za kuinua uwajibikaji na uzalendo kwa nchi yao.

Gratian Mukoba, Rais wa zamani wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), anasema haoni somo hilo jipya likijumuisha elimu ya uraia, bali matukio ya kihistoria yaliyorekodiwa tangu utawala wa kikoloni hadi hivi sasa.

"Sioni kama somo hili jipya la Historia ya Tanzania na Maadili linabeba elimu sahihi ya uraia inayopaswa kufundishwa kwa wanafunzi katika ngazi zote.

"Somo Uraia ni muhimu zaidi katika kuunda jamii inayowajibika na kuleta mbadala wake usiozingatia jambo hilo si sahihi," anasema Mukoba, mwalimu mstaafu.

Kwa mujibu wa mwalimu huyo, Uraia ni somo linalofundisha wajibu wa wananchi kwa taifa lao na haki za msingi wanazopaswa kudai kutoka kwa serikali yao.

Anasema masuala ya kijamii kama vile athari ya rushwa katika uchumi wa nchi, demokrasia, utawala wa sheria na haki za binadamu ambayo watoto lazima wafundishwe kuanzia ngazi ya chini ya elimu yao hayabainishwi vizuri katika muundo wa somo jipya la Historia ya Tanzania na Maadili.

"Huwezi kujenga taifa la watu waliostaarabika na kuwajibika kwa kufundisha tu matukio ya zamani ambayo mengi hayana umuhimu katika mtindo wa maisha wa leo," Mukoba anasema.

Mwalimu huyo aliyekuwa anafundisha masomo Uraia, Historia na Kiingereza katika shule za sekondari kuanzia mwaka 1981 hadi mwaka 2017 alipostaafu, anasema Uraia ni moja ya masomo ya siku nyingi yaliyoanza kufundishwa tangu utawala wa wakoloni.

Hata hivyo, mwalimu huyo anaporejea historia ya elimu nchini, anasema somo hilo lilibadilishwa na somo la Siasa mwaka 1965, yaani mwaka mmoja baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Kwa mujibu wa Mukoba, baada ya Tanzania kupitisha muswada wa marekebisho ya Katiba ya nchi ya mwaka 1984 na mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992, somo Uraia lilirejeshwa kwenye mtaala wa elimu, likifundishwa tena katika shule za msingi na sekondari kuanzia mwaka 1994.

Willbrod Kimaro, mbobevu katika kufundisha somo Uraia, hivi sasa mwalimu wa Shule ya Sekondari Kigamboni, Dar es Salaam, anasema mtaala mpya na sera ya elimu vinaelekeza wanafunzi wa kidato cha kwanza kusoma somo jipya la Historia ya Tanzania na Maadili badala ya Uraia.

"Somo jipya limejikita katika maandalizi ya wananchi wazalendo na waadilifu. Nina matumaini kuwa kutakuwa na kozi za awali za walimu kabla ya kuanza kulifundisha," anasema Kimaro.

Mshauri wa Mambo ya Kitaalamu wa HakiElimu, Dk. Wilberforce Meena, anasema somo jipya la Historia ya Tanzania na Maadili linatilia mkazo zaidi masuala ya maadili kuliko elimu ya uraia.

"Kwa mfano, muhtasari wa somo jipya unaonesha wanafunzi watalazimika kujifunza kuhusu maadili kabla na wakati wa utawala wa kikoloni (1890-1960), baada ya ukoloni (1961-1966), maadili wakati wa Azimio la Arusha 1967-1985 na maadili wakati wa uliberali (1986 hadi hivi sasa," Dk. Meena anasema.

Mshauri huyo anakosoa somo hilo jipya haliambatani na masuala muhimu ambayo yanastahili kufundishwa katika somo Uraia kama vile demokrasia, utawala bora, haki za kijamii, wajibu na haki.

"Uzoefu unaonesha kuwa wizara ya elimu imekuwa na haraka sana katika kuanzisha mawazo mapya, lakini inazembea katika kuweka mazingira wezeshi katika utekelezaji wa mawazo hayo," Dk. Meena anasema.

Hata hivyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo bila kutaja kiasi halisi cha fedha, anasema wizara hiyo katika bajeti ya 2023/24, imetenga fedha kwa ajili ya kuchapisha vitabu vya kiada na kutoa mafunzo kwa walimu wa sasa wa somo Uraia ya jinsi ya kufundisha wanafunzi somo jipya - Historia ya Tanzania na Maadili.

"Hakuna haja ya kuwa na wasiwasi kuhusu mabadiliko haya. Wizara na vyombo vyake vya udhibiti vimeandaliwa vyema. Mchakato wa uandishi na uchapishaji vitabu vya Historia ya Tanzania na Maadili umefanyika kwa umakini mkubwa," anasema Prof. Nombo.

Katibu Mkuu huyo anasisitiza mtaala mpya wa elimu unatekelezwa kwa awamu; ya kwanza itahusisha darasa la awali, la kwanza, la tatu, kidato cha kwanza na kidato cha tano.

Hata hivyo, hadi sasa, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haijatoa taarifa juu ya idadi rasmi ya walimu waliopatiwa mafunzo ya kufundisha somo jipya la Historia ya Tanzania na Maadili katika shule za msingi na sekondari.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Dk. Aneth Komba anasema ofisi yake iko tayari kuchapisha vitabu vya kiada vya kufundishia somo hilo.

"Kuhusu uchapishaji na usambazaji vitabu vya kiada, taasisi inahimiza sana matumizi ya nakala laini. Katika kufanikisha mpango huu, taasisi inashirikisha kampuni tatu za simu ili kuwezesha upatikanaji nyenzo za kujifunzia mtandaoni. Bado tunaendelea na mazungumzo nao na tunatarajia kupata hitimisho zuri," anasema Dk. Komba.

HABARI KITAIFA

# Uwekezaji gesi asilia, mafuta wapaa

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amezindua taarifa za utendaji katika sekta ndogo za umeme, gesi asilia na mafuta kwa mwaka 2022/ na kutoa maelekezo mahsusi kwa wizara na taasisi mbalimbali kufanyia kazi taarifa hizo zinazoonyesha mafanikio na changamoto katika sekta ya nishati.

Akizindua taarifa hizo juzi jijini Dodoma, Dk. Biteko aliziagiza taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati na Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, kusoma taarifa hizo na kuzichambua na changamoto zilizoainishwa zipatiwe majawabu ndani ya miezi mitatu.

Pia aliagiza kuwa kila aina ya fursa iliyoonekana kwenye taarifa hizo, ichukuliwe kwa uzito mkubwa na itambuliwe nani ana uwezo wa kuitumia fursa hiyo ndani ya serikali na taasisi binafsi.

"Vilevile nawaagiza EWURA (Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji) tathmini ya mwaka ujao ihusishe utendaji wa nishati safi ya kupikia ili kujipima kwa usahihi kuhusu utekelezaji wa ajenda hii inayopewa kipaumbele na Rais Samia Suluhu Hassan," alisema.

Aidha, Dk. Biteko aliagiza kuwa matishio yote ya sekta ya nishati yaliyoainishwa katika ripoti kati ya mwaka 2023 na 2025 yapatiwe suluhisho ili katika ripoti ijayo changamoto husika likiwemo suala la kuongezeka kwa mahitaji ya umeme kila mwaka lisiwapo.

Dk. Biteko pia aliitaka EWURA kupima uhusiano wa rasilimali zilizopo na mafanikio ya watu huku akisisitiza kuwa mafanikio ya sekta lazima yaendane na mabadiliko ya maisha ya watu.

Kadhalika, alitaka mifumo ya uagizaji mafuta iendelee kuboreshwa baada ya kufanyika utafiti wa kina na kubainisha kwamba miundombinu ya mafuta bado inahitajika. Aliagiza kuachwa kwa urasimu katika sekta ya nishati.

Dk. Biteko aliipongeza EWURA kwa tathmini ambayo inaonyesha kuwa sekta ya nishati inaendelea kuimarika. Alitoa mfano wa kutolewa kwa leseni ya kuchimba gesi asilia katika kisima cha Ntorya mkoani Mtwara kitakachotoa futi za ujazo milioni 140 kwa siku na kwamba leseni ya mwisho ya kuchimba gesi ilitolewa mwaka 2006.

Kuhusu sekta ndogo ya umeme, alisema serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kuiboresha ukiwamo mradi wa Julius Nyerere (JNHPP) ambao umeingiza mtambo wa pili katika gridi ya taifa kupitia mtambo namba nane, hivyo kufanya kiasi kilichoingia hadi sasa kuwa megawati 470.

"Sekta binafsi imetutoa kimasomaso. Serikali haiwezi kufanya kila kitu, wamefanya kazi kubwa mno kwenye mafuta, gesi na hata kwenye uzalishaji umeme. Wito wangu kwenu msibaki nyuma changamkieni fursa na kwa taasisi zilizo chini ya wizara, msione sekta binafsi kama watu wajanjawajanja, tuwape kipaumbele," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alimshukuru Rais Samia kwa kuiimarisha sekta ya nishati huku akisema Dodoma imeshuhudia matunda ya uimarishaji huo wa sekta kwani sasa umeme haukatiki.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, alisema tathimini iliyozinduliwa inaonyesha sekta imepiga hatua kwenye maeneo megi ikiwamo uhakika wa upatikanaji umeme Pamoja na upatikanaji na usambazaji wa mafuta.

Alisema upatikanaji na uwekezaji wa gesi unaendelea kuimarika ikijumuisha usambazaji gesi kwenye maeneo mbalimbali kama magari, majumbani na viwandani.

Akitoa taarifa za utendaji katika sekta ya nishati, Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dk. James Andilile, alisema sekta hiyo inaendelea kuimarika ikiwamo uwekezaji kwenye miundombinu ya mafuta na uwekezaji wa vituo vya mafuta na maghala. Alisema kwa sasa kuna ongezeko la uagizaji wa gesi ya mitungi (LPG) kwa asilimia 16 na ongezeko la uagizaji wa mafuta kwa asilimia nane.

Dk. Andulile alisema kwa upande wa umeme, uwekezaji umeongezeka katika uzalishaji, usafirishaji na usambazaji huku akibainisha kuwa upotevu wa umeme unazidi kupungua na wateja wameongezeka kutoka milioni 3.8 mwaka 2021/22 hadi milioni 4.4 mwaka 2022/23.

# Naibu Waziri aagiza kasi ujenzi barabara

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, ameiagiza kampuuni ya STECOL inayojenga barabara ya Malagarasi - Ilunde - Uvinza yanye urefu wa kilometa 51.1 kwa kiwango cha lami, kukamilisha kazi hiyo ifikapo Machi 28, mwakani

Kasekenya alitoa agizo hilo juzi mkoani Kigoma huku akimsisitiza mkandarasi huyo kujipanga na kukamilisha mradi huo kwa wakati kwa kuwa mpaka sasa hakuna changamoto yoyote inayokabili mradi huo likiwamo suala la malipo.

"Hakikisha mkandarasi unakamilisha kuweka lami kilometa 44 zilizobaki kati ya 51. Hatutegemei baada ya kipindi hicho wana kigoma wawe wanapita kwenye vumbi. Naamini utamaliza kwa wakati kwani kila kitu unacho," alisema Kasekenya kama alivyokaririwa kwenye taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano Serikali cha Wizara ya Ujenzi.

Pia alimwagiza Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Kigoma, Mhandisi Narcis Choma, kumsimamia mkandarasi huyo kujenga barabara hiyo kwa ubora na kujiridhisha kila hatua ya utekelezaji.

Naibu Waziri alitolea mfano wa barabara ya Chagu - Malagarasi ambayo imejengwa kwa ubora kwa kuwa ina miaka 10 tangu kujengwa kwake na haina kiraka wala shimo lolote hadi sasa.

Kasekenya pia alitoa rai kwa wananchi wa Kigoma na watumiaji wa barabara hiyo kuhakikisha wanatunza na kulinda alama za barabarani zitakazowekwa na kutojihusisha na vitendo vya wizi wa alama hizo kwani kufanya hivyo kunaweza kusababisha ajali na pia kuitia hasara serikali.

Meneja Miradi wa STECOL, Cao XiaoJun, alimhakikishia Naibu Waziri Kasekenya kufanya kazi usiku na mchana pamoja na kuongeza wafanyakazi ili kukamikisha mradi huo kama walivyoagizwa.

Alisema mradi kwa sasa umefika asilimia 52 ukihusisha kazi mbalimbali ikiwamo kuweka tabaka la lami kilometa saba, kujenga makalavati madogo na makubwa, kuweka tabaka la kokoto kilometa tisa na kuweka tabaka la udongo uliochanganywa na saruji kilometa 13.

Mradi huo umefadhiliwa na serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Mfuko wa Abu Dhabi na OPEC na unajengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 73.

# Vijana wasomi waonywa kutumika kisiasa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) mkoani hapa, kimeonya vijana wasomi wasikubali kutumika na kurubuniwa na wenye fedha katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu unaotarajia kufanyika 2025.

Katibu wa Siasa na Uenezi wa CCM Mkoa wa Singida, Elphas Lwaji, alisema hayo jana wakati akizungumza kwenye kikao cha viongozi wa matawi ya CCM ya vyuo na Vyuo Vikuu Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Mkoa wa Singida.

"Kipindi hiki cha uchaguzi ni kipindi cha kutumia fedha sana, msitumike vibaya na watu wenye fedha na mkawaambie wazee na wazazi wenu wasikubali kununuliwa, wachague viongozi wazuri ambao watasaidia nchi kuleta maendeleo," alisema.

Lwaji alisema wasomi wana nafasi kubwa ya kutoa ushauri kwa wanaoteua wagombea waweze kuteua watu wazuri ambao wakichaguliwa watakuwa chachu ya kuleta maendeleo, badala ya kusubiri kuja kulaumu kuchagua kiongozi asiyefaa.

"Tunaona kabisa huyu mbunge hatatufaa, huyu mwenyekiti wa mtaa hatatufaa, huyu mwenyekiti wa kijiji hatatufaa halafu mnanyamaza kimya, hapana twendeni tukawashauri wazee wetu wachague viongozi sahihi na makini," alisema.

Lwaji aliwataka vijana kujitokeza kujiandikisha katika daftari la kudumu la mpiga kura ili wawe na nafasi nzuri ya kushiriki kupiga kura wakati wa uchaguzi.

Alisema viongozi wa matawi katika vyuo na vyuo vikuu wahakikishe wanahamasisha watu waweze kujiunga katika chama sanjari na kulipa ada ya uwanachama.

"Ili uweze kusajiriwa kidijitali ni lazima uwe na kadi ya CCM, na ili uwe mwanachama hai lazima ulipie kadi ya uanachama maana huwezi kuwa kiongozi kama huna wanachama wengi kwenye eneo lako," alisema.

Lwaji aliwataka wasomi hao kutumia mitandao ya kijamii vizuri kwa ajili ya kujifunza kwa kuwa nchi inawategemea kuja kuwa viongozi wazuri wa baadaye.

Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Singida Mjini, Mohamed Msaghaa, alisema wasomi ndio kundi ambalo linapima na kuchakata mambo hivyo wanategemewa ili kuwa viongozi bora.

Mlezi wa Seneti Mkoa wa Singida, Salum Kanyungu, aliwakumbusha wanavyuo ambao ni wanachama wa CCM umuhimu wa kuzingatia maadili na nidhamu.



Mamalishe akiandaa ugali kwaajili ya wateja wake, katika eneo la Mwenge Maryland, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam jana. Ugali ni moja ya chakula kikuu na cha asili kinachopendwa na waafrika wengi. **PICHA: JOHN BADI**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu ya malipo mtandao ihusishe wananchi wote

**WAZIRI** wa Fedha, Dk,. Mwigulu nchemba, Alhamisi wiki hii, aliwasilisha mapendekezo ya mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka 2024/25 jijini Dodoma. Katika mapendekezo hayo, serikali imepanga kutumia Sh. trilioni 49.35 kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa shughuli za serikali na miradi ya maendeleo.

Baada ya kuwasilishwa kwa mapendekezo hayo, wabunge kuanzia Jumanne wanatarajia kujadili na hatimaye kupitishwa na kwa mujibu wa kanuni za bunge, ili bajeti ipite, inatakiwa mbunge kupiga kura kwa kusema NDIYO au HAPANA.

Kwa kawaida, hakuna bajeti ya serikali iliyowahi kukwama kwa wabunge kuikataa isipokuwa makadirio ya mapato na matumizi ya zilizokuwa wizara za miundombinu, na nishati na madini wakati wa serikali ya awamu ya nne, kwa mawaziri husika kutakiwa wakajipange upya kutokana na kukosa uhalisia.

Wakati wa kuwasilisha mapendekezo hayo ambayo bajeti ya mwaka ujao wa fedha imepokewa kwa hisia chanya na Watanzania wengi, mkazo mkubwa alioutoa Waziri Nchemba ni kuongeza ukusanyaji mapato kwa ajili ya kupata fedha zitakazowezesha serikali kutekeleza miradi mingi ya maendeleo ya shughuli za kila siku ikiwamo ulipaji wa mishahara na stahiki kwa watumishi wa umma.

Katika kusisitiza hilo, Dk. Nchemba alisema nguvu kubwa itaelekezwa katika matumizi ya risiti na malipo ya kidijitali kwenye miamala mbalimbali. Hatua hiyo itasaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti kuvuja kwa mapato ya serikali, hivyo kuwezesha kuongezeka kwa fedha katika mfuko wa serikali.

Licha ya kusisitiza mfumo huo, Waziri Nchemba pia alisema watahimiza malipo mengi ya serikali kufanyika kwa njia ya mtandao tofauti na sasa ambapo mfumo wa malipo ni kwa fedha taslimu.

Mkazo mkubwa katika hilo ni kuwezesha kuwapo kwa usalama wa fedha za wananchi na serikali kwa ujumla pamoja na kuendana na mabadiliko ya sasa ya sayansi na teknolojia ambayo yanahusisha pia miamala mbalimbali.

Lengo la kufanya hivyo, alisema ni kuwa na mfumo wa uchumi usiotumia fedha taslimu (cash less economy) ambao pia unaokoa muda wa mtu kufanya miamala popote alipo bila kwenda benki au kununua bidhaa sehemu fulani.

Kwa kutumia mfumo huo, mtu anaweza kulipia bidhaa au huduma kama vile kukata tiketi ya ndege, meli au gari bila Kwenda kwenye ofisi husika.

Wazo la kufanya malipo kwa njia ya mtandao ni jema kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia ambayo ni mfumo wa kidunia na Tanzania haiwezi kujitenga.

Wahenga wanasema maendeleo hayo yaliyochagizwa na utandawazi ni sawa na mafuriko ambayo mtu hawezi kuyazua kwa kutumia viganja vya mikono yake. Kwa mantiki hiyo, Watanzania watake wasitake ni lazima wakubali na kuwa katika mfumo rasmi.

Pamoja na ukweli huo, kwa sasa ni Watanzania wachache wanaotumia mifumo rasmi ya huduma za kifedha kama vile benki na malipo kwa njia ya mitandao ya simu.

Kutokana na hali hiyo, elimu kuhusu matumizi ya kifedha kwa njia jumuishi inapaswa kutolewa kwa wananchi wote ili kushiriki kikamilifu katika hilo.

Kama ambavyo hivi karibuni timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Fedha wakishirikina na maofisa wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wamekuwa wakipita mikoani kutoa elimu kuhusu mikopo maarufu kama kausha damu au mikopo umiza, suala la malipo mtandao halina budi kupewa kipaumbele.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Uchaguzi unakuja, vijana msikubali kutumiwa na wanasiasa

Na Sabato Kasika

**VIJANA** ni nguvu kazi ya taifa, hivyo ndivyo iilivyo, ili nguvukazi hiyo iweze kuzaa matunda, ni muhimu vijana wenyewe wajitambue wajue wajibu wao na watumike kwa manufaa yao na ya umma.

Pamoja na kwamba wao ni nguvukazi ya taifa au taifa la kesho, bado wako baadhi yao ambao huwa wanatumiwa vibaya na wanasiasa hasa wakati wa kampeni za uchaguzi kwa kufanya vurugu au fujo.

Kimsingi, mwamko wa vijana unaendelea kukua kadri miaka inavyokwenda, hasa kutokana na hamasa zinazotokana na makundi mbalimbali yakiwamo ya wanasiasa na wanaharakati.

Ni zaidi ya miaka 30 sasa tangu vijana waanze kuhamasika kwenye siasa baada ya uchaguzi wa mwaka 1995 ambao baadhi yao walifukuzwa vyuoni baada ya kubainika kuwa wanashabikia siasa.

Lakini mwamko huo, kumekuwapo baadhi yao ambao kama nilivyoeleza awali kuwa hutumiwa na wanasiasa kwa manufaa ya hao wanaowatuma, kitendo ambacho ni wazi wanajiharibia mbele ya jamii.

Mwaka huu ni wa uchaguzi wa serikali za mitaa, ingekuwa ni vyema vijana wasikubali kutumika, badala yake wawe mstari wa mbele kuufanya uchaguzi huo kuwa wa amani na utulivu.

Isiwe kama ambavyo imewahi kutokea miaka ya nyuma kufuatia baadhi ya vijana kushiriki vurugu kwa kushambuliana na wenzao wa vyama vingine wakati wa kuelekea au kutoka kwenye kampeni.

Kuwapo kwa vurugu au fujo huku viongozi wao wakiwa kimya bila kukemea, ni wazi wanatumika vibaya. Hivyo ninadhani ni vyema sasa vijana kuamka na kujua haki na wajibu wao katika uchaguzi.

Miongoni mwa haki na wajibu ni kuchagua na kuchaguliwa, si kushiriki katika matukio ya kuharibu uchaguzi, kwa lengo la kunufaisha wale waliowatuma na kuwaneemesha, huku wao wakiibaki kama walivyo.

Ni haki yao kujiunga na vyama hasa kwa wale waliotumiza umri wa miaka 18, lakini kukubali kutumiwa na wanasiasa badala ya kuandaliwa kuwa viongozi wa baadaye, si sahihi.

Siasa, uongozi, na utawala ni mada ambazo zinaweza kuwa ngumu kuzungumza juu yake kwani zinahusisha masuala magumu ya kijamii, kiuchumi na kisiasa, hivyo ni muhimu kufanya siasa kwa umakini.

Ni muhimu kuelewa kuwa siasa, uongozi, na utawala vina uhusiano wa karibu. Siasa ni mchakato wa kuunda sera na maamuzi ambayo yanashughulikia masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Lakini pia, uongozi ni uwezo wa kushawishi watu kufuata maamuzi yako na kufanya kazi pamoja kufikia malengo fulani. Utawala ni mchakato wa kutekeleza sera na maamuzi ambayo yamechukuliwa.

Ni vyema wanasiasa wakatumia njia hiyo ya kushawishi watu kufuata maamuzi yao ambayo ni sahihi kwa manufaa yao, jamii na taifa kwa ujumla, badala ya kushawishi kufanya vurugu au fujo.

Vilevile, ni vyema wanasiasa wajue kuwa siasa, uongozi, utawala na uwajibikaji ni mambo muhimu katika kuendesha jamii na taifa. kwa kusimamia na kuongoza masuala hayo kwa njia nzuri.

Njia hiyo nzuri ni kutoshirikisha vijana katika vurugu ili kupata uongozi, bali inawezekana kujenga na kuandaa vijana imara, ambao wanaandaliwa kuwa viongozi bora wa taifa la kesho.

Hivyo, ingekuwa ni vyema vyama vya siasa kuanza kuendelea kuwaandaa vijana wao ambao ninadhani kwamba wanaweza kuwa viongozi ili washiriki katika uchaguzi ujao.

Wasiwe watu wa kukubali kushiriki kwenye matendo ambayo si mema ndani ya jamii, kwani kuwashirikisha kwenye vurugu ni sawa na kuwandaa kuwa watu wasiofaa katika jamii.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Nguzo saba za mafanikio kupitia 'manifestation'



Pascal Mayalla

KWA wasomaji wapya, wiki iliyopita nilitoa utangulizi wa mada iitwayo "manifestation". Kwa lugha rahisi ,ni kuweka nia na kudhamiria kwa dhati kufanikiwa, kwa kutumia nguvu na nia zilizomo ndani mwako.

Katika Makala hiyo, nilidokeza kwamba 'manifestation' ina nguzo kuu saba ambazo ni msingi (foundation); sheria; mitetemo; kuweka nia; kuweka kwa jicho la ndani; kutumia Imani Chanya ya kufanikiwa; na utekelezaji.

Nguzo kuu ya kwanza ndiyo msingi mkuu wa 'manifestation' na ni nia na imani ya kufanikiwa. Kwa msingi huo, kuna makundi makuu matano ya watu waliofanikiwa. Kundi la kwanza ni warithi (inheritors). Hawa ni watu waliozaliwa kwenye familia tajiri, wafalme na matajiri na viongozi. Mtoto wa familia hii anazaliwa na kujikuta amerithi utajiri hata kama kichwani ni sifuri. Huyu atahesabika amefanikiwa.

Kundi la pili ni la watu akili nzuri (the best brains). Hawa ni watu wenye akili nzuri, wasomi na wataajiriwa kazi nzuri, na kulipwa mishahara, hivyo kupata maisha ya mafanikio. Kwa kiasi kikubwa, kundi hili ni la waajiriwa.

Wenye vipaji ni kundi la tatu katika waliofanikiwa. Hili ni kundi la watu kama wanamuziki, wasanii, waigizaji, wacheza mpira, au watu wenye vipaji vyovyote vinavyowaletea maisha mazuri, wakiwemo waandishi wa Habari na watangazaji. Mwanamuziki Michael Jackson hakusoma hata darasa moja!, Diamond Platnum wetu, Harmonize ni darasa la saba tu lakini wamefanikiwa kutokana na vipaji.

Wanaofanya kazi kwa bidi (hard workers) ni kundi lingine. Kufanya kazi kwao kwa bidi na maarifa kumewafanya wafanikiwe kimaisha. Kwa vyovyote vile, ukifanya kazi kwa bidii utafanikiwa. Hili ni kundi la wanaofanikiwa kwa kutumia nguvu zao, "mtaji wa masikini ni nguvu zake".

Kundi la mwisho ni wapigadomo (fixers). Katika kundi hili kuna wanasiasa, wanaweza wasiwe na akili nzuri, vipaji vyovyote, hawafanyi kazi kwa bidi lakini wanafanikiwa kwa kupiga domo, kupiga dili, kufanya mizengwe na kuuza lugha.

Makundi yote hayo yanafanikiwa kwa kufanya 'manifestation' kwa kujua au bila kujua.

Lugha nyingine ya 'manifestation' kuifanya njozi yako kuwa kweli.

Msingi mkuu wa manifestation ni nia na imani ya kujiamini kuwa wewe una nguvu ndani yako na una uwezo wa kufanikiwa kwa kutumia mawazo yako kutia nia ya kuzifungulia hizo nguvu zilizomo ndani yako zikuletee mafanikio ya kupata kitu unachokitaka

'Manifestation' ni kutumia nguvu ya Mawazo kupitia fikra Chanya kwa kufungua nguvu na karama iliyoko katika mawazo yako kukuiwezesha ikupec kile unachokitaka. Watu wote wenye mafanikio wanatumia 'manifestation' kwa kujua au kutokujua lakini siri kuu ya kwanza ya mafanikio ni kuwa na ndoto, wazo, nia, kisha kuifanyia kazi ndoto yako .

Kuna wengi wana mawazo mazuri tu ya maendeleo na kusema "nikiwa mkubwa nataka kuwa rubani, daktari, polisi au mfanyabiashara" lakini wazo hilo linaishia hewani kwa sababu hulifanyii kazi. Ili ufanikiwe, ni lazima ufanyie kazi ndoto yako. Kuota tu ndoto ya unataka kuwa Tajiri bila kuifanyia kazi ndoto hiyo inaitwa 'ndoto ya mchana' kama ile hadithi ya ndoto ya alinacha kwenye hadithi za Alfu Lela Ulela.

Kwenye nguzo saba za 'manifestation', nguzo ya kwanza ni asili. Kuna wengi wanadhani 'manifestation' ni jambo jipya lakini si kweli kwa kuwa ni jambo la enzi na enzi toka enzi za Masihi, alifundisha: "Ombeni mtapewa, bisheni mtafunguliwa" na akasema "ukiwa na imani kama chembe ya haradali, unaweza kuiambia milima iondoke na milima ikahama".

Kitu kinachoitwa 'meditation', tafakuri jadidi au tahajudi ni 'manifestation'. Wakati wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani, Waislamu wanatakiwa kunuizia kufunga kila siku kuwa kesho nitafunga. Kitendo cha kunuizia ni 'manifestation'. Wakatoliki hufanya sala za Novena, hiyo pia ni manifestation. Sala za kujirudia rudia kama rozali ni 'manifestation' na sala za tasbihi ni 'manifestation'.

Mara nyingi enzi za ujana maji ya moto, mvulana akimwona msichana, akampenda, akadhamiria kumpata, hufanya juhudi mbalimbali ili kumpata, hivyo kutumia 'manifestation' bila kujijua lakini mwisho hufanikiwa.

Ili kupata mafanikio kwenye jambo lolote lazima, kwanza, uwe na ndoto ya kufanikiwa. Ndoto hiyo ni kuwa na mawazo chanya, kwa kizungu 'positive thinking'. Mawazo chanya haya yanakuwa yana nguvu ndani yake, kisha uweke nia thabiti na ya dhati ya kufanikiwa na mwisho ufanye juhudi na bidii kulifanikisha hilo jambo lako. Ile nguvu iliyomo ndani yako, itafungua milango ya mafanikio na utafanikiwa.

Kuna watu wanadhani kuna watu wana bahati tu ya kufanikiwa na wengine wana laana ya umasikini, jambo hilo halipo. Mungu alimwumba binadamu ili afanikiwe lakini kuna kanuni za mafanikio. Ukizifuata na kuzipatia ni lazima utafanikiwa.

Wiki ijayo nitakuletea nguzo ya pili ya 'manifestation' yenye sheria 12 za mafanikio ambazo ukizifuata kikamilifu lazima utafanikiwa.

**Paskali**
**+255 754 270403**

# Wadau wapongeza serikali kwa udhibiti bei ya sukari

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kipindi cha hivi karibuni, tasnia ya sukari nchini imekuwa ikikumbwa na changamoto nyingi, hususan suala la bei kupanda holela.

Baadhi ya viwanda vya sukari viliongeza bei ya sukari na kukataa kushusha licha ya kupata msaada wote kutoka kwa serikali ili kuongeza uzalishaji.

Hali hii ilifikia kilele wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhani, ambapo bei ya sukari ilipanda kutoka Sh. 2,500 kwa hadi 6000 kwa kilo katika maeneo mbalimbali. Pia baadhi kutokana na bei hiyo, ilionekana nafuu ilipokuwa ikiuzwa Sh. 4,000. Hatua hiyo ilisababisha malalamiko mengi kutoka kwa wananchi.

Kutokana na hali hiyo, serikali iliamua kuchukua hatua kali ili kudhibiti kupnda kwa bei ya bidhaa iyo adhimu kwa kutoa vibali vya uagizaji wa sukari kwa wafanyabiashara wengine sokoni.

Hatua hii ilileta matokeo chanya kwa kuwa bei za sukari zilianza kushuka kutoka Sh. 4,000 hadi Sh. 2,800 kwa kilo moja.

Hata hivyo, serikali iliona haja ya kuchukua hatua zaidi kwa kupelekwa muswada wa sheria bungeni ili kuvunja ukiritimba wa viwanda vya sukari.

Kwa manufaa ya wamiliki matajiri watano wa viwanda vya sukari, serikali ilioona haiwezi kushikilia mateka watu wake milioni 65 na wakaendelea kuumia na bei ya sukari.

Kwa lengo la kushinikiza serikali kubatilisha mabadiliko hayo, wamiliki wa viwanda hivyo walirejea katika vitendo vyao vya kifisadi kwa kuhonga baadhi ya wanasiasa wapige kelele dhidi ya hatua hizi nzuri za serikali.

Ni nini kibaya ikiwa kampuni ndogo au kubwa ziliruhusiwa kuagiza na kuuza sukari sokoni ili kushusha bei? Je, ni kampuni kubwa pekee ndizo zinazostahili fursa ya kuagiza na kuuza sukari?

Swali la kujiuliza, je, baadhi ya watu wanataka serikali isichukue hatua yoyote huku makundi ya kifisadi yakiendelea kuwanyonya wananchi wake?

Ni dhahiri kuwa tatizo hili lingeachwa bila kudhibitiwa, gharama kwa uchumi ingekuwa kubwa sana.

Mfumuko wa bei ya sukari ungeathiri sekta mbalimbali za uchumi na ingesababisha kuongeza gharama za maisha kwa wananchi na kupunguza uwezo wa kununua bidhaa nyingine muhimu.

Hii ingeweza kusababisha madhara makubwa kwa ustawi wa kiuchumi wa taifa.

Ni wakati wa kusema hapana kwa hujuma na kulinda maslahi ya wananchi na kwa kuwa serikali ipo kwa ajili ya wananchi na iendele kuhakikisha haki inatendeka kwa wote.

**KAULI ZA WADAU**

Idd Salum, mkazi wa Tandika, Dar es Salaam, anasema serikali imefanya jambo jema kwa kuingilia kati suala la sukari na kuruhusu wafanyabiashara wengine kuagiza bidha hiyo ili kuondoa ukiritimba.

"Zikiachwa kampuni kubwa mbili tu kuagiza sukari tutakuwa tunarudi kule kule bidhaa hii itaadimika na bei itapanda kwa hiyo hatua ya serikali kuingilia kati na kuruhusu kampuni ndogo na kubwa kuagiza sukari ni jambo la neema sana kwa Watanzania," anasema.

Mmoja wa wafanyabiashra wa sukari Tandika, Haule Shangu, anasema biashara ya sukari isiachwe kwa kundi dogo kwa kuwa kufanya hivyo wanaweza kutumia nafasi hiyo kuwaumiza wananchi.

Anasema biashara ya sukari ina fedha nyingi kwa hiyo serikali inapaswa kuiangalia kwa jicho la kipekee kwani watu wachache wanataka kujimilikisha sekta hiyo ili kucheza na bei wanavyotaka.

"Kwanza, napongeza hatua ambazo serikali ilichukua baada ya kubaini kuwa watu wachache wanaweza kucheza na bei ya sukari na kuamua kuruhusu kampuni zingine kuagiza sukari naomba mwendo uwe huo huo kampuni nyingine ziruhusiwe ili watu wachache wasiwe na uwezo wa kucheza na bei ya sukari," anasema.



Kuadimika kwa sukari, kumefanya baadhi ya wafanyabiashara kunufaika kwa kupandisha bei. **PICHA: MAKTABA**

# HABARI PICHANI



Mkuu wa mkoa wa Manyara, Queen Sendiga akichangia damu, wakati wa sherehe za kuadhimisha miaka 20 ya uchangiaji damu, mjini Babati juzi, ambapo chupa 1,512 sawa na asilimia 142.67 zilipatikana. **PICHA: GIFT THADEY**



Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Mkoa wa Dar es Salaam, Nasra Ramadhani, akizungumza na waandishi wa habari mkoani humo jana, akiiomba Serikali kuifungia mitandao ya Twitter na X, akidai inatumiwa vibaya kwa kusambaza baadhi ya habari au taarifa za upotoshaji na zisizo na ukweli. **PICHA: JU-**



Wachuuzi wa machungwa wakiyashusha kutoka kwenye lori na kuyapanga kwa viwango vya bei, katika Soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. Chungwa moja, linauzwa kuanzia 40/- hadi 50/-, kwa bei ya jumla. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mwenyekiti wa shirika lisilo la kiserikali la Saidia Wanajamii Tanzania (SAWATA), Mohamed Mghanja, akizungumza kuhusu jamii kusaidia wahitaji, baada ya kampuni ya uchimbaji madini ya Heroes, kutoa msaada wa vyakula mbalimbali kwa watoto yatima wa mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**



Kazi ya upanuzi wa barabara ya Morogoro kutoka eneo la Kimara Mwisho hadi Ubungo, ikiendelea mkoani Dar as Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# MAISHA

JUNI 16, 2024

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 14

**Salad isiyopikwa**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Fanya uchaguzi sahihi wa sakafu ya nyumba



Ukurasa 12

**HARUSI**





# 'MESENJA BEGI' Ni Zaidi ya mkoba

Ukurasa 13

# WATOTO


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| U | ■ | S | H | I | N | A |
| D | ■ | ■ | ■ | M | ■ | N |
| I | ■ | D | U | A | ■ | Z |
| W | A | O | ■ | R | A | I |
| A | ■ | N | I | A | ■ | S |
| N | ■ | D | ■ | ■ | ■ | H |
| I | B | A | R | A | ■ | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

ZAA, MIA, TII, NAE, MBATA, MEZWA, SIMBA, AMANI, ASHINDE, UBINGWA


## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

TAFUTA MAUMBO HAYA KATIKA MCHORO ULIOPO HAPO CHINI.






## PAKA RANGI




## CHEKA



### Alichokifanya daktari

MTOTO Juma na ragiki yake John walikuwa wakitembea pembeni ya barabara wakielekea shambani. Wakati wakikaribia shambani, Juma alimuona ndege akipaa angani huku akiyumbayumba kwa madaha.Juma alifurahi sana na kuanza kumuuliza rafiki yake.

**Juma:** Ona yule ndege anaruka kwa furaha

**John:** Nimefurahi baba kasema ukumuona ndege ana furaha atakuwa na makinda.

**Juma:** Kwani ndege sawa na mnazi una makinda?

**John:** Hapana ila watoto wa ndege wanaitwa makinda na sio mnazi.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Ndoa yako ikifuatiliwa na nguvu za giza ufanye nini?

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada yetu ya wiki iliyopita ikidodosa dalili kuwa ndoa yako inafuatiliwa na nguvu za giza. Nilitaja chache nikaahidi kumalizia zingine leo.

Naam. Dalili nyingine ni pale heshima aliyokuwa nayo mke/mume wako mbele za watu inapungua. Anakuwa hakupi uzito mbele za watu.

Ukiona kuwa zamani wakati mnaoana mke/mume wako alikuwa hana tabia ya kubishana na wewe mbele za watu na sasa amekuwa akifanya hivyo hata haoni aibu kuwa anachokifanya siyo sahihi, ujue kuwa mnahitaji msaada wa karibu sana kuinusuru hiyo ndoa yenu.

Dalili nyingine ni pale mnapobishana na kugombana kwa kitu kile kile kila mara. Kunapokuwa na hali ya kutokuelewana kwa mambo yale yale kwenye ndoa kwa muda mrefu bila kupata suluhu ya kudumu kunaweza kusababisha ndoa kufa!

Kwenye ndoa nyingi huwa kunatokea migongano ya aina nyingi. Mfano, kuna watu wanapoingia kwenye agano la ndoa, wenzi wao huwa wanawashauri kuweka mipaka ya kuwa karibu na baadhi ya watu waliokuwa na mazoea nao pale zamani. Hii ni kwa ajili ya kulinda ndoa zao!

> **"Pale unapogundua kuwa wewe mara zote unakuwa wa mwisho kujua chochote cha muhimu kinachomhusu yeye. Zamani mwenzako alikushirikisha vitu vyake lakini sasa hafanyi hivyo, hayo ni mabadiliko lazima uweke alama ya kuuliza/mshangao.**

Pale mke/mume anapoacha kuheshimu hisia na mawazo ya wenzi wake aliyoyatoa kwa muda mrefu, shida huanza kutokea, na mgogoro huo kama haitapatikana hekima toka pande zote, ndoa hiyo inaweza kuingia kwenye hatari ya kufa.

Ipo dalili pale mmoja wenu au wote kwa pamoja hajisikii hamu ya kusogeleana mnapolala. Tendo la ndoa ndio kitu pekee kinachofanya ndoa iendelee kuwa hai.

Pale tu wanandoa wanapofikia kwenye hatua ya kuchokana wanapokuwa pamoja, ujue kuna hatari ya ndoa hiyo kufa. Kwani kila mtu anaweza kuwaza kutafuta mtu mwingine nje ya ndoa.

Dalili nyingine ni pale unapojikuta kuwa ni wewe peke yako ndiye unayehusika katika kutatua migogoro au matatizo ya ndoa. Kila ndoa huwa inapitia changamoto na majaribu mbalimbali. Wanandoa wenye uhusiano mzuri huwa wanashirikiana kupatia ufumbuzi matatizo yao.

Kwa mfano, mke au mume anapokuwa na matatizo ya uzazi, kwa kawaida wote wanatakiwa kuwa na umoja ili kupata suluhu la hilo tatizo lao. Lakini pale unapoona ni wewe peke yako aidha mke au mume unashughulika peke yako kupata ufumbuzi na mwenzako hafuatilii wala chochote kuhusu afya yako muda mrefu, jua ya kuwa ndoa yako ipo hatarini.

Unapoona wewe peke yako ndiye unayeshughulikia kutafuta fedha kuhudumia familia na mwenzako hajali chochote, na wala hakutii moyo wa kuendelea mbele, ujue ndoa ipo hatarini kufa.

Pale unapogundua kuwa wewe mara zote unakuwa wa mwisho kujua chochote cha muhimu kinachomhusu yeye. Zamani mwenzako alikushirikisha vitu vyake lakini sasa hafanyi hivyo, hayo ni mabadiliko lazima uweke alama ya kuuliza/mshangao.

Au mambo yake muhimu anawaambia wengine kabla yako au wakati mwingine hakushirikishi kabisa, unatakiwa utafute msaada kuokoa ndoa yako ili isizikwe.

Pale unapogundua kuna mambo mengi mabaya yanayofanyika kwenye ndoa yako kuliko mazuri. Hapa wanandoa hujikuta wakitupiana lawama kila mara, huku wakipishana ndani ya nyumba bila kusemeshana, lugha za ukali kila mara, hasira na kutishiana kuachana.

Haya yakiendelea kujirudia, jua ya kuwa unahitaji msaada mkubwa wa ushauri na maombi. Maana ndoa isiyokuwa na amani ni sawa na jehanamu ndogo hapa duniani.

Mpenzi msomaji, bila shaka umepata kujua dalili mbalimbali zinazoonyesha kuwa ndoa yako inashambuliwa na nguvu za giza. Zipo nyingi ila hizo ni kwa uchache.

Sasa unaweza kuuliza, nifanye nini ndoa yangu inaposhambuliwa na nguvu za giza? Ni muhimu sana kufanya maombi ya kufunga siku 21 kumsihi Mungu arejeshe ndoa yenu kwa upya.

Pia maombi ya vita ni muhimu dhidi ya roho zilizoachiliwa kuua ndoa za watu. Vile vile maombi ya mapatano kama wanandoa. Mungu anaheshimu ndoa. Wanandoa wanapoomba pamoja shetani hawezi kuivunja hiyo ndoa.

Pia zipo roho za mizimu kazi yao kubwa ni kutenganisha ndoa. Omba kwa kudhamiria kwa imani kubwa. Beba silaha zote za Mungu uweze kushinda mipango yote ya ki-shetani na mawakala wake.

Tuishie hapa.

**Una maoni, Kisa? Ujumbe 0715268581. Naomba hii pia ipo WhatsApp tuma maoni yako.**

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Kwa talaka hizi, tutegemee ongezeko la 'single mothers'

UCHUNGU ni nini? Ni hisia abebazo mtu baada ya kufikwa na jambo au maudhi fulani. Ni mwitikio wa kihisia uliosababishwa na tukio lililomkosesha mtu amani moyoni.

Kwa maneno mengine, uchungu ni ishara ya awali inayoonyesha kuwa kuna jambo lililosababisha uchungu moyoni. Inawezekana kabisa huwa ni jambo lililoshindikana kuachia/kushindwa kusamehe.

Kwa hiyo unapoutazama uchungu kwa mtazamo huo, utaona kwamba uchungu ni kifungo mtu hujifunga kitokana na hali alizopitia zenye kusababisha uchungu moyoni. Ndiyo maana uchungu humuondoa mtu katika nafasi aliyonayo.

Kwa nini nimeanza waraka huu na suala la uchungu. Jibu ni jepesi tu kwamba ninajaribu kuunganisha kila nukta na kauli ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji), Prof. Kitila Mkumbo kuhusu talaka.

Alhamisi wiki hii, wakati akiwasilisha taarifa ya hali ya uchumi wa taifa kwa mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 Bungeni Jijini Dodoma, alisema Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), umesajili hati za talaka 866 mwaka 2023, ikilinganishwa na hati za talaka 447 zilizosajiliwa mwaka 2022.

Kwa mujibu wa RITA, hati za viapo vya ndoa 45,455 zimesajiliwa ikilinganishwa na hati 51,011 mwaka 2022.

Sasa hivi iko kasumba ya vijana kutotaka kuoa na wengine kuolewa, wakiishia kuamini kuwa single mother ni bora zaidi ya kuishi na mume.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971; mwenye majukumu ya kisheria ya kutunza mwenzake kwenye ndoa ni mwanaume. Mwanamume anapaswa kumlisha, kumvisha, kumtibu na kumjengea mke au wake zake.

Isipokuwa mwanamke, atafanya tu pale ambapo mume atakapokuwa hawezi tena kufanya kazi kutokana na ajali au magonjwa au changamoto zingine.

> **Sasa hivi iko kasumba ya vijana kutotaka kuoa na wengine kuolewa, wakiishia kuamini kuwa single mother ni bora zaidi ya kuishi na mume.**

Anakuheshimu lakini hakunyenyekei. Sasa dada zangu kosa kubwa nikuwa wakishapenda wananyenyekea, wanakubali kila kitu hata vitu vingine vya kijinga. Wanafanya hivyo si kwakupenda lakini wanaogopa kuachwa.

Hilo ndilo kosa kumfanyia mwanamume kila kitu, kwa kua unaogopa kuachwa, ndiyo sababu utaachwa au utateseka katika mahusiano yako yote.

Unachotakiwa kufanya ni kumheshimu lakini si kumuogopa wala kumnyenyekea. Kama kitu huwezi kufanya mwambie hiki hapana, mwambie nakupenda ila hili hapana.

Kingine, Sheria ya Ndoa, Sura ya 29 ya mwaka 1971 kama ilivyorekebishwa mwaka 2019, ni sheria kuu inayosimamia masuala ya ndoa nchini Tanzania.

Hata hivyo, sheria hii ni moja kati ya sheria kongwe nchini Tanzania na imekabiliwa na changamoto nyingi, ambazo ni pamoja na; kuruhusu mazingira fulani ya ubaguzi wa kijinsia kwa wanawake na wasichana.

Kwa mfano, inawabagua wavulana na wasichana katika uwezo wa kuingia katika ndoa.

Pili, mnapaswa kujua Sheria ya ndoa, ina utata katika suala la ugawaji wa mali za ndoa wakati wa talaka hasa katika ndoa za mitala.

Vilevile, sheria hii inatoa wajibu kwa mume tu kutoa mahitaji kwa ajili ya familia, na imeshindwa kutoa tafsiri na adhabu juu ya masuala ya ukatili hasa wa majumbani.

Upungufu na changamoto zilizoko katika sheria hii zinaleta mkanganyiko katika kusimamia na kutafsiri masuala yanayohusu ndoa nchini Tanzania.

*•Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com Simu ya mkononi: +255 715 545 490*

# HARUSI









Kumbukumbu iliyotukuka kwa wanandoa Godson Mafita na Theopista Mzena, wakati walipofunga ndoa miaka minane iliyopita katika kanisa la Calvary Asemblies of God jijini Dodoma.

# MITINDO







## ‘MESENJA BEGI’

# Ni Zaidi ya mkoba

Kama wewe ni mjasiriamali au mfanyakazi katika ofisi tofauti na umechoka kubeba mabegi mikononi? Basi kuna mbadala wa kufanya nalo ni kutumia mabegi yenye mikanda mirefu maarufu kama ‘Messenger Bag’.

Begi hizi zimeleta mapinduzi ya ubebaji nyaraka au vifaa kwa urahisi na wakati huo huo inakupa mwonekano mzuri wakati unapotembea nalo.

Kawaida begi la aina hii hutengenezwa kwa kutumia malighafi za asili au feki, na kisha linavalishwa kamba kwa ajili ya kuweka juu ya bega moja na kamba lake inakaa katika kifua ili begi ikae mbele au nyuma.

Begi hili linafaa sababu sio tu kwa matumizi ya ofisini, kama wewe ni mwanafunzi wa chuo au mjasiriamali litakusaidia kubeba baadhi ya vitu vyako muhimu.

Wabunifu wameongeza thamani kwa kuweka nakshi mbalimbali kama mifuko ya nje, zipu na hata vifungo vya sumaku

Pamoja na urahisi wake, hizi begi haijalishi nguo unayovaa kwani zinapendeza na vazi lolote utakaloamua kuvaa,

UREMBO

Na Mary Geofrey

# ZUIA MIDOMO ISIPASUKE

MIDOMO ni sehemu muhimu ya kiungo kwa binadamu kutokana na jukumu lake kubwa la kusaidia kumeng'enya chakula na mwonekano unaopendeza.

Leo tutaelekezana kuhusu njia za kukusaidia kuzifanya midomo yako isipauke au kukatika katika kipindi hiki cha baridi.

Kwa kawaida midomo inapopasuka husababisha kupunguza mwonekano mzuri hasa wa wanawake.

**Mambo ya kuzingatia**

Hakikisha unatumia vilainishi vya midomo ambavyo vitakuwa kinga na kuzuia mionzi ya jua inayoweza kusababisha ukakatika.

Usilainishe midomo yako kwa kutumia ulimi kwasababu mate husababisha kuendelea kuongeza ukavu na kukatika kwa midomo.

Epuka kutumia rangi ya midomo ambazo zina chembechembe za vilevi kwasababu husababisha midomo kuwa mikavu.

Hakikisha unakunywa maji ya kutosha na juisi ili kuongeza unyevunyevu wa maji ndani ya mwili na lips kuwa laini wakati wote.





MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Salad isiyopikwa

SALADI isiyopikwa ni aina ya chakula kinachotokana na mbogamboga ambazo haziwezi kuliwa bila kupikwa.

**Mahitaji**

Kabeji moja kubwa, lettuce kifungu kimoja, karoti tatu kubwa, pilipili manga vijiko viwili vidogo, matango mawili makubwa, pilipili hoho mbili ndogo, mayonnaise nusu kijiko, kitunguu kimoja kikubwa, limao au siki vijiko viwili vidogo.

**Maandalizi**

Osha kila mboga, menya maganda, katakata kabeji, lettuce, karoti, na hoho.

**Namna ya kutengeneza**

Pasha pamoja kabeji, lettuce, karoti, hoho na uweke chumvi. (dakika 5 tu). Wakati huo katakata tango na kitunguu kisha changanya na chukua mayonise changanya na pilpili manga.

Epua zile kabeji kisha acha halafu anza kuchanganya kabeji na mchanganyiko wa tango na kitunguu. Weka limao, mayonnaise yenye pilipili manga na tango lingine kwaajili ya kunakshi.

Tayari saladi yako itakuwa imekamilika kwa ajili ya kula na chakula ukipendacho.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

## Tumia ukuta kutuliza akili yako

Na Restuta James

NYUMBANI ni sehemu inayopaswa kumpa mtu utulivu na kumwondolea msongo wa mawazo wa mizunguko na kazi za kutwa nzima, ndio maana kila eneo la nyumba linapaswa kuweka utulivu unaokusudiwa.

Baadhi ya wanasaikolojia wanashauri aina za maua ya kupanda na mpangilio wa vitu ambao unachochea utulivu kulingana na mwonekano wake baada ya kupangwa.

Akizungumza na Nipashe mapema wiki hii, mtaalamu wa rangi za nyumba, Tumaini Jonathan, anasema ukuta unaweza kutumika kueleza hisia ambazo mwenye nyumba akiona anapata utulivu na kumpunguzia msongo wa mawazo.

Anasema unaweza kuweka mchoro wa ua au mti wowote unaoupenda ambao ukiuona unakupa hali ya utulivu.

"Unaweza kutengeneza mchoro wa mgomba, ua au mti wowote, unaweza kupaka rangi unayoipenda pia sio lazima kijani. Inaweza kuwa rangi ya dhahabu au nyingine kulingana na mapenzi ya mtu," anasema.

Anashauri kwamba mchoro huo ambao unaweza kuwa kama pambo mahsusi, unapaswa kuwekwa kwenye ukuta ambao 'unaonekana sana' pindi mtu anapoingia au kutoka ndani.

"Kwa kuwa nia yake ni kutuliza ubongo au kuamsha hisia za furaha, ni vyema mchoro ukawekwa kwenye ukuta unaoonekana kwa urahisi," anasema.







# Fanya uchaguzi sahihi wa sakafu ya nyumba

KARIBU ndugu msomaji wa safu hii inayohusu masuala ya nyumba. Kila uchapo tunashuhudia mabadiliko yanayojitokeza maishani ambayo kwa namna mbalimbali yanasababishwa na maisha ya utandawazi tuliyo nayo katika karne ya sasa.

Mambo yaliyofanyika jana si yale yanayofanyika leo na hayatafanyika kesho wala keshokutwa. Kila siku yanaibuliwa mambo mapya au kwa mtindo mwingine au kwa ubora zaidi endapo yaliwahi kufanywa.

Na leo tunaangalia ubora ulioko sasa katika uwekaji wa sakafu ndani ya nyumba.

Katika nyumba, sakafu ni moja ya vitu vinavyochangia kupendezesha nyumba na hata pale inaposakafiwa kwa utaalamu mzuri.

> "Japokuwa tunashauri kwamba usiwe nyuma ya wakati sana, hakikisha ni bora lakini inaendana na wakati," anasisitiza.

Yako baadhi ya mambo yanayopaswa kuzingatiwa kabla ya kusakafia nyumba ambayo msanifu majengo, David Kashozi, anayaeleza kuwa kabla ya kuweka sakafu, ni muhimu kuangalia rangi ya nyumba ili visipishane sana.

Jambo la pili ambalo anasema linapaswa kuzingatiwa wakati wa kufanya uchaguzi wa sakafu ni ubora wake. Jambo la tatu ni kuchagua sakafu ambayo ni rafiki na salama kwa makundi yote ya watu wanaoishi katika nyumba yako.


"Chagua sakafu ambayo haitawakwaza baadhi ya watu kulingana na umri wao hususani watoto, wazee na wagonjwa, maana nyingine zina utelezi mkali," anasema Kashozi.

Jambo la nne, anasema ni vizuri kuzingatia kuchagua sakafu ambayo ni bora na inadumu kulingana na bajeti uliyojiwekea kabla ya kubadili nyingine.

"Japokuwa tunashauri kwamba usiwe nyuma ya wakati sana, hakikisha ni bora lakini inaendana na wakati," anasisitiza.

Na jambo la tano, anashauri kwamba ni vema kufanya maandalizi mapema ya aina ya sakafu unayoitaka.

# HABARI PICHANI



## HABARI KIMATAIFA

# Rais Ramaphosa ataka serikali mpya kujibu matatizo ya wengi

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, amekuwa katika mtihani wa kutimiza matakwa ya raia wake baada ya kuchaguliwa na bunge kuendelea na nafasi yake kwa awamu ya pili.

Kuchaguliwa kwake kushika nafasi hiyo kunatokana na chama chake cha African National Congress (ANC) kuingia makubaliano na vyama vya upinzani kuunda serikali ya umoja wa kitaifa.

Serikali hiyo mpya inachanganya ANC, Muungano wa mrengo wa kati wa Democratic Alliance (DA) na vyama vidogo.

Katika hotuba yake ya ushindi, Rais Ramaphosa alipongeza muungano huo mpya na kusema wapiga kura wanatarajia viongozi kuchukua hatua na kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya kila raia.

Makubaliano hayo yaliharakishwa ili kupisha Bunge kuanza vikao vyake ikiwamo kuthibitisha kwa kura ni nani angeshika madaraka katika utawala huo mpya.

Makubaliano yalifikiwa baada ya wiki kadhaa za uvumi kuhusu chama gani kingeshirikiana na ANC baada ya kupoteza wingi wa wabunge kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 30 kwa kupata asilimia 40 ya kura katika uchaguzi uliofanyika mwezi uliopita.

Chama cha DA kilishika nafasi ya pili kwa kujinyakulia asilimia 22 ya kura zote.

Katibu mkuu wa ANC, Fikile Mbalula, aliutaja muungano kuwa ni hatua ya kushangaza.

Kauli hiyo alimaanisha Rais Ramaphosa, ambaye alichukua nafasi hiyo kwa rais wa zamani Jacob Zuma baada ya kuwepo mgogoro, kufanikiwa kushika kiti hicho tena tofauti na viongozi waliomtangulia.

Hatua inayofuata ni Rais Ramaphosa, kuunda baraza la mawaziri ambalo litajumuisha chama cha DA na vyama vingine vishiriki.

Serikali hiyo haitahusisha vyama viwili vilivyojitenga na ANC, ambavyo ni Umkhonto Wesizwe (MK) kilichoundwa na Jacob Zuma na Economic Freedom Fighters (EFF) kinachongozwa na Julius Malema.

Huenda vyama hivyo vitanufaika iwapo umoja huo utashindwa kuleta uboreshaji wa kiuchumi unaodaiwa na wapiga kura.

Wakati huo huo, viongozi wa muungano wa nchi za BRICS ikiwemo China na Urusi, wamempongeza rais Ramaphosa kwa kuteuliwa kuongoza nchi hiyo kwa muhula mwengine wa miaka mitano.

Rais wa Russia, Vladimir Putin, katika ujumbe wake wa kumpongeza Ramaphosa, alisema anamshukuru kwa mchango wake katika kuimarisha ushirikiano wa mataifa hayo mawili hasa katika Umoja wa Mataifa, kundi la G20 na muungano wa Bricks.

Katika upande mwengine, Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, alipongeza rais Ramaphosa kwa uteuzi wake, ikisifia juhudi za taifa hilo kujaribu kuhakikisha amani inapatikana nchini mwake.

Ramaphosa aliingia madarakani kwa mara ya kwanza mwaka wa 2018 baada ya rais wa zamani Zuma kuondolewa kwa madai ya ufisadi.

Chini ya uongozi wake, nchi hiyo imekuwa ikikabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo kukatika kwa umeme mara kwa mara pamoja na kudorora kwa uchumi wa taifa.

**BBC.**



Waumini wa dini ya Kiislam wakiwa katika kisimamo cha Arafat katika kukaribisha ibada ya hija nchini Saudia Arabia jana.
**PICHA: DPA**

# Marekani yaifunga bandari ya Gaza

**WASHINGTON,** MAREKANI

JESHI la Marekani limesema hali mbaya ya hewa katika bahari imesababisha kusitishwa kwa muda shughuli ya upakuaji wa misaada katika gati la muda lilojengwa Gaza.

Taarifa kutoka Kamandi Kuu ya jeshi (CENTCOM) ilisema hali gati hilo linatumika kupitisha misaada ya kibinadamu kuingia eneo la Ukanda wa Gaza.

Kupitia mtandao wa x, CENTCOM, ilisema kwamba gati hilo litaelekezwa katika bandari ya kusini mwa Israel ya Ashdod, na uamuzi huo umechukuliwa ili kuzuia uharibifu wa miundombinu unaosababishwa na kuchafuka kwa bahari.

Ilisema hatua ya kuhamishwa ili liweze kuendelea kutoa huduma zaidi katika siku za usoni.

Taarifa ya Kamandi hiyo imeongeza kwamba gati hilo litarejeshwa katika ufuo wa Gaza mara tu hali ya hewa itakapotengemaa.

Bandari hiyo ya muda inatumika kama kitovu cha usambazaji wa misaada muhimu inayohitajika Ukanda wa Gaza tangu Mei 17, zaidi ya tani 3,500 zimepitia eneo hilo.

**DW**

# Raia Afrika ya Kati waajiriwa kupigana vita nchini Sudan

**NEWYORK,** MAREKANI

Uchunguzi wa Umoja wa Mataifa umeonyesha kuwa vikosi vya kijeshi vya Sudan vinalitumia taifa la Jamhuri ya Afrika ya Kati kama sehemu ya kuajiri watu kwa ajili ya kwenda kupigana nchini humo.

Katika ripoti iliyotolewa na kamati ya wataalamu iliyoundwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, ilioonyesha wasiwasi kuhusu athari za ziada zinazotokana na mzozo huo kwa kueleza nchi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati imeathirika na mzozo unaoendelea nchini Sudan.

Ripoti ya kamati hiyo iliangalia masuala kadhaa ikiwemo hali ya kiutu wakati nchi hiyo ikishuhudia wimbi la mamilioni ya wakimbizi kutoka Sudan.

Pia iliangazia uvamizi wa pande mbili zinazohasimiana pamoja na matumizi ya anga kwa jeshi la Sudan karibu na kituo cha mpakani cha Umm Dafog ambacho ni kitovu cha wanamgambo wa RSF.

Aidha wataalamu hao wa Umoja wa Mataifa wameitolea wito serikali ya Afrika ya Kati kukabiliana na ongezeko la biashara haramu ya silaha kutoka mataifa jirani hasa nchini Sudan.

**DW**

# Rais wa zamani afutiwa kinga

**NIAMEY,** NIGER

MAHAKAMA ya Niger, imeondoa kinga kwa rais aliyeondolewa madarakani, Mohamed Bazoum, na kufungua njia ya uwezekano wa kukabiliwa na kesi

Bazoum aliondolewa madarakati katika mapinduzi ya kijeshi yaliyofanyika Julai, 2023.

"Mahakama imeagiza kuondolewa kinga kwa Mohamed Bazoum," alisema jaji mkuu wa mahakama ya juu, Abdou Dan Galadima.

Serikali ya Niger inamshutumu rais huyo aliyeondolewa madarakani kwa kula njama ya kuhatarisha usalama na jaribio la kuyumbisha usalama wa taifa, uhaini, ugaidi na kufadhili ugaidi.

MBazoum anazuiliwa tangu alipopinduliwa katika makazi ya rais, akiwa na mkewe Hadiza. ilikuwa imeahirishwa mara mbili, mawakili wa Bw. Bazoum wakiwa wameshutumu vizuizi kadhaa vya haki ya utetezi.

**RFI**

## MAKALA

# OMBWE LA UONGOZI AFRIKA LINASABABISHA UMASIKINI



Na Magabilo Masambu

**Watu wengi duniani hutaka wanavyoviona au wanayoyaona kupitia macho yao. Wachache sana huona wanayoyataka akilini katika fikra zao, hivyo watu hawa ndio wameleta teknolojia, mabadiliko makubwa ya kisayansi na mambo mengi muhimu yaonekanayo leo kwa macho katika ulimwengu.**

KUELEKEA uchaguzi wa Serikali za mitaa baadaye mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani, tujikumbushe machache kuhusu viongozi wetu.

Nchi nyingi za kiafrika zimekuwa haziendelei kwa sababu nyingi za kiutawala. Moja ya sababu kubwa zaidi ni kukosa viongozi bora wenye uamuzi chanya na msimamo juu ya kutetea na kulinda mali za bara letu.

Pili, viongozi hao wameshindwa kuwa na maono ya kitaifa ya muda mrefu na yenye tija katika kujenga uchumi imara. Tatu, kukosa uzalendo wa hali ya juu ambao ndio msingi wa uongozi bora ili kuleta maendeleo ya kweli kwa taifa.

Sifa ya kiongozi bora ni kuwa na maono ya kuona njia ya kutatua matatizo makubwa na yaliyoshindikana kwa wananchi wake.

Kiongozi wa namna hii, hasubiri maoni ya wengi juu ya jambo ambalo anaona ni muhimu kwa watu wake ili mradi liwe jema kwa nchi, hivyo kujitosa na wachache walioelewa umuhimu wa jambo lenyewe na baadaye, wengi huelewa umuhimu wake baada ya lengo kutimia kama lilivyokusudiwa na kuonekana kwa watu wote kuwa lina maslahi kwa taifa.

Sifa kubwa ya kiongozi ni kuona njia. Wanaoongozwa wengi huwa hawaoni njia, hivyo akiwauliza juu ya anachokiona yeye ambapo wengine hawaoni kitu, inawezekana ikawa ngumu sana watu hao kuamini kiongozi anachokiona, hivyo kushindwa kufikia lengo. Kutokana na ukweli huo, kiongozi bora huamua kufanya mambo ya msingi bila kujali wangapi wataelewa umuhimu wa shughuli anayoiamua bali hutambua fika kuwa wengi watamwelewa baada ya matokeo.

Watu wengi duniani hutaka wanavyoviona au wanayoyaona kupitia macho yao. Wachache sana huona wanayoyataka akilini katika fikra zao, hivyo watu hawa ndio wameleta teknolojia, mabadiliko makubwa ya kisayansi na mambo mengi muhimu yaonekanayo leo kwa macho katika ulimwengu.

Mfano, aliyeunda gari aliona alichokitaka katika akili na fikra zake na aliiona picha ya gari akilini likitembea barabarani na kwamba siku moja litumiwe na watu wote.

Kama angelichukua hatua ya kuwaomba maoni juu ya kile alichokiona akilini, hakika gari lisingewezekana. Wengi wangelisema unachowaza hakitawezekana, hivyo gari lingebakia kichwani mwa yule aliyewaza. Lakini aliyenunua lile gari alipenda alichokiona kwa macho yake.

Hebu fikiria ulishawahi kujiuliza kwa nini uliwahi kuwachukia walimu wako darasani kila walipokuadhibu umekosea na kuwaona kama maadui zako? Jibu ni kwamba uliwachukia kwa sababu hukujua kuwa walikutakia mema zaidi katika kukuandaa kimaisha na kuishi vizuri.

Walimu walilazimika kutumia nguvu na viboko zaidi bila wewe kuelewa nia yao njema na tayari leo baada ya kufanikiwa, ndipo umeelewa lengo la walimu juu ya maisha yako na kubakia kuwashukuru kwa kusema bila mwalimu fulani leo nisingefika hapa nilipo.

Viongozi wanapaswa kwanza wawe na uwezo mkubwa katika kupambanua faida na hasara ya mambo katika nchi.

Hali hiyo itawafanya waanze kuelewa mambo muhimu ya kimaendeleo ambayo wana wajibu wa kuyafanya bila wengine kuelewa kusudi.

Kusudi litaonekana baada ya kufanyika mambo hayo na kuleta maendeleo kwa wananchi wote yanayoonekana.

Watu makini huona fursa ya mwanga katikati ya giza nene, wakati huo wengine huona kero katikati ya giza nene. Kwa maana hiyo, watu wengi hawaamini kuwa inawezekana hivyo ukiwasikiliza ushauri wao maranyingi hupoteza.

Israel iliona fursa katikati ya ukame mkubwa na jangwa lililoenea nchi nzima.

Wakachimba visima virefu na kuwekeza katika kilimo cha matunda na leo ndiyo nchi pekee inayosambaza matunda duniani kote. Lakini uamuzi huo ulifanywa na viongozi makini tu wenye maono yenye tija kwa taifa.

Kinyume cha haya yote, itakuwa bahati mbaya sana kama tutapata viongozi ambao watakuwa na maono ya kuyaingiza mataifa yetu matatizoni kwa manufaa yao binafsi na ya muda mfupi.

Kelele nyingi za Waafrika juu ya viongozi wao, zimekuwa zikiashiria kwamba wako baadhi ambao wanawaza kwa niaba ya wananchi lakini wakikusudia kujinufaisha binafsi na kwamba kila atakayekuja huko mbele atajijua. Wenzetu Ulaya ukiwa kiongozi, unawaza na ajaye aongoze vipi ili yale mliyokubaliana kama nchi yaendelee kusimamiwa.

Ushauri wangu kwa viongozi wetu wote, wawe na maono au mawazo ya watu tunaowaongoza ni muhimu kuhakikisha kwamba, yote kwa pamoja yalenge kulijenga taifa.

Lakini viongozi mnayo nafasi zaidi ya kutazama ni mambo gani yatakayowafaa wananchi na mataifa yetu kwa ujumla.

Tumewapeni dhamana ya kuongoza kwa niaba yetu siyo badala yetu na hivyo tunategemea maamzi yenu yawe na nia njema kabisa na mataifa yetu.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar es salaam-Tanzania**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Chura upunguze vituko, kuku na yai kilianza nini?*



Na Adam Fungamwango

**Pamoja na kumiliki wanamuziki wenye vipaji vya hali juu, lilitoa nyimbo nyingi zilizotikisa na kupendwa mno miaka ya 1980. Kwenye miaka ya 1970, mbali na nyimbo nyingi tamu za taarabu, wimbo uliokuwa bora kabisa wakati huo ulikuwa 'Sabarkheri Mpenzi' ambao ulivuma kama moto nyikani.**

CHURA ninakuuliza unipe jibu makini kwa kila ijapo mvua wakimbilia bwawani. Huna nguo ya kufua na wala huna sabuni, nijibu yapate tua, maji utayafanyani.

Chura punguza vituko na wako uhayawani, umezua sokomoko watu hawaelewani. Ukivunjika mgongo, dawa atakupa nani?"

Ni baadhi ya maneno maarufu yaliyomo kwenye kibao cha taarabu kilichotikisa mwanzoni hadi mwishoni mwa miaka ya 1980.

Yoyote yule aliyekuwa mtoto, kijana au mkubwa kwenye miaka hiyo sidhani kama hataufahamu wimbo huu.

Mara kwa mara ulikuwa ukipigwa na kuimbwa na wasikilizaji wengi kwenye redio ya taifa kwa sasa, wakati huo ikiitwa, Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD).

Ni moja ya nyimbo bora kabisa za muziki wa taarabu asilia enzi hizo zilizowahi kutokea.

Ulipigwa na kundi la JKT Taarab, ukiimbwa na Patricia Hillary. JKT Taarab lilikuwa moja ya makundi bora kabisa wakati huo ya muziki huo.

Pamoja na kumiliki wanamuziki wenye vipaji vya hali juu, lilitoa nyimbo nyingi zilizotikisa na kupendwa mno miaka ya 1980.

Kwenye miaka ya 1970, mbali na nyimbo nyingi tamu za taarabu, wimbo uliokuwa bora kabisa wakati huo ulikuwa 'Sabarkheri Mpenzi' ambao ulivuma kama moto nyikani.

Ni wimbo ambao hadi wasanii wa kizazi cha sasa wamekuwa wakiurudia kwa mitindo mbalimbali.

Hata wasanii Aslay na Nandy juzi juzi tu waliurudia. Ukweli tu ni kwamba, wimbo huo ambao asili yake ni Zanzibar, walirudiwa na wanamuziki wengi sana.

Ikaja miaka ya 1980, ambapo kulikuja na mapinduzi makubwa ya muziki wa taarabu, hasa Tanzania Bara.

Kuliundwa makundi mengi, na wengi wa wanamuziki walikuwa wanachukuliwa kutoka Zanzibar na Tanga ambapo kiasili, inasemekana ndiko kwenye wasanii wazuri zaidi wa muziki huo, ingawa hata mikoa mingine baadaye walitokea wengi wakawa mahiri sana.

Wanamuziki wa Taarabu wa Tanzania, wakavuka nchi hadi Burundi ambako walikwenda kuunda makundi mawili hasimu, Shaan Musical Club, na Jasimine Musical Club, ambayo nayo hayakushikika kwa kutoa nyimbo zilizotokea kuwa bora, si Burundi tu, bali Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Muongo mzima wa 1980, makundi yalishusha nyimbo kwa kushindana. JKT Taarab wakatoa wimbo wa 'Mdudu ndani ya kokwa la embe kaingiaje', halafu wakarudi tena na wimbo wa 'Kuku na Yai' kinachouliza kuku na yai nini kilianza. Huu uliimbwa na Elizabeth Sijila.

Egyption Music Taarab kutoka Zanzibar wakadondoka na wimbo huo 'Pendo Linaua', ukiimbwa na Afua Selemani, Bima Taarab nao hawakukubali, wakalipa na wimbo wa 'Tunapendana kwa Dhati'.

'Ni bure zenu fitina, sisi wala hatuzijali. Wenyewe tumependana, kuachana ni muhali.' Yalikuwa ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye kibao hicho, kilichoimbwa na marehemu Mariam Naylon. JKT Taarab kama kawaida yao, wakashuka na wimbo 'Ukewenza'.

'Somo aliyenifunza mafunzo nazingatia, Siogopi ukewenza mume akishaamua, katu sijajikimbiza, mwenzangu kumkimbia, nitamtunza mume wangu kama ilivyo sheria, nizidishe penzi langu, mapeshi kunisifia, nije mpiku mwenzangu na mbwembwe kumtilia.

Mume akishaamua kuweka ukewenza, katu usije kimbia, mwenzako atajikweza.' Maneno haya yamo kwenye wimbo huo.

Patricia, alirudi tena na wimbo 'Njiwa peleka salamu' namba moja ambao ulikuwa maarufu, halafu baadaye akatoa namba mbili yenye maneno yafuatayo;-

"Njiwa usimlaumu kosa ni wako muhibu, njiwa kampa salamu yeye akamgilibu."

JKT Taarab hawakupoa, wakaja na wimbo 'Jamani Mapenzi Yananitatiza' mwimbaji Patricia, lakini pia wakampa Sijila wimbo wa 'Nahodha kukaa Nyuma.'

Dhamira Musical Club, wakaja wakawa na wimbo wa 'Kifo cha Mama' na 'Kilio cha Baba'.

Kikundi kidogo cha Makutano Dancin Troupe cha Manzese Uzuri, kilikuwa na taarabu yao, kikarekodi wimbo ulioondokelea kuwa maarufu 'Siku yako ipo Nimekuwekea.'

"Siku yako ipo mwanangu nimewekea, ukishageuka upepo usije kulia, kuna siku iso jina, zamu yako itafika, usidhani nyongo sina ewe swahiba pulika, utendayo nayaona lakini nayalimbika, siku yako iko mwanagutu nimekuwekea utapogeuka upepo usije kulia,

Siku hiyo utanuna kama hujapatacheka, na mafunda kukutuna lau kama utapasuka, mito utaitafuna uzirarue na shuka." Ni wimbo uliotikisa mno.

Shaan wao walitoa wimbo maarufu wa 'Sina Zaidi ya Wewe', Jasmine wao wakajibu wa wimbo wa 'Pendo kazi Yetu.'

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Harufu ya Panya-12

KIJANA Heri alikutana na msichana Nuru katika duka fulani maeneo ya Chanika, Dar es Salaam. Baada ya kuongea waliyoongea wakakubaliana kuonana siku ya Jumapili kwenye nyumba ambayo alimuelekeza aje kuulizia. Siku ilifika kama walivyoahidiana, masaa machache kabla ya kuwasili Heri alianza kusikia harufu mbaya chumbani kwake, ambayo kwa uzoefu wake aligundua ni ya panya aliyekufa. Akafanya kila kitu ambacho alidhani kinaweza kumaliza tatizo kwani muda ulivyozidi kusonga mbele ndiyo harufu nayo ilizidi. Muda wa Nuru kufika ulikaribia. Njia mbadala aliyotumia kuondoa harufu ndiyo iliyoleta balaa zaidi.

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)

MAMBO yaliyotokea wiki iliyopita yakawekwa pembeni. Kile kilichoshindwa kufanyika wiki iliyopita kikafanyika siku hiyo.

"Unajua pamoja na kukufuata wewe, lakini pia namhitaji mzee raia kwa ajili ya jambo letu lile." Nuru alimkumbusha baada ya kutoka bafuni kujimwagia maji.

Wiki iliyopita, alikwenda kuoga yeye kwanza, ili mwenzake aje baadaye, ila mambo yalivurugika alipomkuta ameshapandisha. Siku hiyo walikwenda kuoga wote.

Heri akakumbuka mazungumzo ya wiki iliyopita kati ya Nuru na mzee Raia.

"Mzee mimi ni msichana mdogo sana, wala sipendi haya madudu, yameniingia mimi mwenyewe nikiwa sijui. Na aliyesababisha haya yote ni mama wa kambo, hakuwa mtu mzuri kabisa..."

"Basi basi mama, leo usiongee sana maana bado hauko kwenye hali ya kawaida, unabidi ukapumzike nyumbani, ila baada ya wiki moja urudi hapa ili tulimalize hili tatizo."

"Yaani mzee kama unaweza kulimaliza mimi nitashukuru sana, maana rafiki zangu wameshawahi kunipeleka maeneo tofauti lakini imeshindikana. Mimi sitaki hali hii, nataka niwe mzima kabisa."

"Nitaliondoa hilo tatizo, tena bure, sitaki hata pesa yako, huyu mwenzako ni rafiki yangu sana, huwa tunakutana njiani na tunaongea sana, ingawa nilikuwa sijawahi kufika kwake na yeye kwangu, leo hii alifika kwa sababu alinihitaji." Akakumbuka.

"Ndiyo nakumbuka hilo. Sasa sijui twende wote kwake, au niende nikamwite!" "Mhh! Kwenda wote bado, ujue mimi nahitaji matibabu kutoka kwake. Hapa ndipo panafaa siyo kwake kila mtu ajue."

Wazo hilo likaungwa mkono na Heri. "Basi pumzika nikamwite."

********************************

Mzee Raia na Heri waliingia chumbani na kumkuta Nuru amekaa kitandani. Ni kwamba ndani ya chumba hakuna kochi, hivyo mara nyingi mwenyewe au mgeni maalum hukaa kitandani, lakini huwa na kigoda ambacho hukaliwa na mgeni wa heshima.

Mzee Raia akapewa kigoda, Heri mwenyewe akachua mkeka akatandika chini na kukaa, Nuru akiachwa kitandani.

Hata hivyo alinyanyuka na kwenda kumlaki mzee. "Shikamoo mzee wangu." Akamwamkia kwa bashasha kiasi cha kumfurahisha mzee Raia. Kukumbatiwa kwake ilikuwa heshima kubwa. Aliona analipwa heshima kutokana na kile alichokifanya wiki iliyopita.




"Mzee mimi ni msichana mdogo sana, wala sipendi haya madudu, yameniingia mimi mwenyewe nikiwa sijui. Na aliyesababisha haya yote ni mama wa kambo, hakuwa mtu mzuri kabisa..."

"Marahaba mwanangu." Akaitikia kwa furaha. Alikuwa amekuja na kikapu chake, ambacho kuna vitu aliweka ndani.

Baada ya makaribisho kila mmoja alitazamia kuzungumzwa kile kilichohitaji kuzungumzwa.

"Enhee Nuru, mzee Raia huyu hapa nimemleta, ulimhitaji kutaka kuzungumza naye, karibu." Heri akavunja ukimya. Alikuwa na furaha isiyomithilika, kumpata msichana kama Nuru, ambaye alionekana kumhusudu siku ile ya kwanza alipomuona dukani, maeneo ya Chanika.

Akakohoa kidogo, kwa aibu za kike, akaimanisha kichwa chini kidogo, halafu akaanza kwa sauti nyembamba, nyororo na ya kubembeleza.

"Mzee wangu kwanza ahsante sana kwa yote ambayo umenifanyia wiki iliyopita. Nimeongea na shangazi yangu akashangaa sana. Kwanza mpaka sasa haamini kama kuna mtu anaweza kutibu maradhi yangu..."

"Ulimwambia kama ulikuja kwangu, nikawasha udi, ukapandisha..." Akadakia Heri na kusababisha vicheko.

"Walaaa!" Akajibu Nuru, baada ya kumaliza kucheka, huku akipandisha bega lake la upande wa kushoto, kuonyesha kukataa. "Nilidanganya nimeenda kwa shoga yangu, baba yake alikuwa amechoma udi, nikapandisha, shangazi anajua kuwa mimi nikinusa tu pafyumu kwa dakika moja mfululizo, napandisha, hata udi. Kwa hiyo nikamwambia baba yake shoga yangu ndiye aliyelishusha dude, na akaniambia anaweza kuliondoa. Akashangaa sana, na akaniambia hawezi. Nikamwambia kasema anaweza. Akaniruhusu, amesema kama anaweza sawa, lakini ana wasiwasi kutokana na jinsi nilivyotupiwa hili jini."

"Enhee nilitaka kuuliza hapo hapo, kuwa ilikuwaje hadi likakuingia, maana hilo jini lako, linaitwa Anzura. Hili kazi yake likimwingia binadamu ni kumzuia kuoa kwa mwanaume na kuolewa upande wa mwanamke. Utakuta mwanaume anaishi peke yake, wazazi marafiki wanamshauri aoe, wapi. Yeye anataka aendelee kufanya uhuni. Na hata akiwa na wazo hilo, baadaye ataghaili. Kwa watoto wa kile hivyo hivyo, atakataa wanaume, na wanaomtaka kumuoa ambao yeye atawakubali, mipango inakaa vizuri, baadaye wanamkimbia." Mzee Raia akafafanua halafu akaendelea "Utalijuaje? Yakitokea mazingira kama yake yaliyokupata ndiyo linajitokeza, na kwa bahati mbaya sana lilikuja wakati upo kwa mpenzi wako, likakasirika, linaona wivu, likaona kama kuna mpango wa kutaka kuolewa, ndiyo likapiga mkwara ule."

"Mimi nilizaliwa Muheza, Tanga." Nuru akaanza kuhadithia. "Nilipofika umri wa miaka tisa, mama yangu akafariki na baadaye baba yangu akaoa mke mwingine. Huyo mama alikuwa na mabinti wawili mapacha, ambao baba yangu aliwalea. Baba yangu hakuwa na tabia ya kukaa sana nyumbani kutokana na kazi yake ya udereva wa malori ya kwenda nchi za nje. Mama yangu wa kambo akaona hii ni fursa ya kuninyanyasa na kunitesa. Niliteswa mimi. Napewa kazi si saizi yangu, wakati mwingine nashindishwa na njaa wakati chakula nimekipika mwenyewe. Nilikuwa naogopa kumwambia baba anaporejea. Niliteseka sana kusema kweli."

"Pole sana." Mzee Raia alisema huku akitikisa kichwa. Heri hakusema lolote. Ilionekana kama yanayosemwa yamemwingia hadi amejisahau.

"Tulipokuwa wasichana wakubwa sasa, watu wengi walikuja kutaka kunioa. Hawakuwa wakimkuta baba. Walimkuta mama. Kuna waliokuja tu kuahidi kwa mdomo, wengine waliléta barua kabisa, lakini mama alikuwa anazichanachana na kuwarudishia pesa zao. Watoto wake hawakupata bahati hiyo kwa sababu walikuwa jeuri, hawana kauli nzuri kwa watu. Wavivu, hata kupika hawajui. Sifa zote zilikuja kwangu mimi, kwa sababu mwanzo waliona kama wananitesa, lakini nilijua kumbe walikuwa wananipa mafunzo mazuri kwa maisha yangu ya baadaye. Kila mtu alikuwa ananisifia sio uzuri tu, tabia, kujituma kwenye kazi, hata mapishi."

"Basi leo hapa huondoki bila kutupikia." Heri akadakiwa kwa mara ya kwanza tangu Nuru alipoanza kutoa historia yake na kusababisha wenzake waangue vicheko.

"Kanunue mahitaji tu baba, utaomba kila siku niwe hapa, au nisiondoke kabisa." Akajibu Nuru na kufanya vicheko viongezeke. "Enhee, lete habari." Mzee Raia alimhimiza kuendelee.

"Basi, yule mama wa kambo baada ya kuona mabinti zake hawapati bahati ya kuuliziwa kuchumbiwa, alizidi kunichukia, maneno mama, nasikia ndiyo akaenda kwa watu wabaya sijui wachawi, nikatupiwa jini.

Niwaambie tu kubwa ya hapo kila kitu kikawa ovyo, nikaanza kuumwa, waliotaka kunioa, wote wakakimbia, kila mtu ananiona sifai. Shangazi yangu alilitambua hilo, akaja kunichukua akanileta Dar es Salaam. Lakini alihangaika kila kona. Kamaliza waganga wote, lakini hakuna kitu. Mwisho akajiamulia kukaa tu."

ITAENDELEA JUMAPILI

# SHAKIRA JIMBO LIKO WAZI

MWANAMUZIKI maarufu wa Marekani, Shakira, ametoa nafasi kwa mwanaume mwingine baada ya kuachana na mwanasoka Gerard Pique.

Shakira amesema kwa sasa yuko tayari kuanzisha uhusiano na mwanaume mwingine.

Msanii huyo anayesifika kwa uchezaji wake wa kukatika, alisisitiza kwamba uhusiano huo mpya ulenge ustawi wa watoto wake.

Ameeleza kwamba ushiriki wowote wa kimapenzi utahitaji kuzingatia utayari wao wa kihisia na kisaikolojia.




# OMONDI AMPOTEZA MDOGO WAKE

MSANII wa vichekesho maarufu wa Kenya, Eric Omondi, amekuwa katika hali ya majonzi baada ya mdogo wake, Fred Omondi, kupoteza maisha katika ajali ya gari.

Fred aliaga dunia jana asubuhi baada ya gari lake kupata ajali katika barabara ya Outering, jijini Nairobi.

Kwenye ukurasa wake wa Instagra, Eric alichapisha video ya wimbo wake wa kuikejeli serikali ambao aliumbia na mdogo wake huyo.

"Nenda vizuri kaka @fredomondi_," Eric amendika chini ya video hiyo.



## ZISIKUPITE

### OLISE AWA LULU ULAYA

KLABU za Newcastle na Bayern Munich zilikuwa klabu za kwanza kuwasiliana na Crystal Palace zikitaka kumsajili winga Mfaransa Michael Olise mwenye miaka 22. (**Athletic**)

### ....CHELSEA WAJITOSA

CHELSEA nao wamefuta mpango wao kuwasiliana na Palace kuhusu Michael Olise. (**Mirror**)

### NONI MADUEKE AWINDWA

MCHEZAJI wa kimataifa wa England chini ya umri wa miaka 22 anayeichezea Chelsea, Noni Madueke pia yuko kwenye orodha ya wanaowaniwa na Newcastle huku klabu hiyo ikiwa na mpango wa kumnunua winga mpya wakati dirisha la uhamisho wa wachezaji litakapofunguliwa. (**i Sport**)

### VAN DIJK AWANIWA

KLABU ya Al Nassr inayoshiriki Ligi ya Saudia, inataka kumfanya beki wa Liverpool na timu ya taifa ya Uholanzi, Virgil van Dijk kuwa beki anayelipwa fedha nyingi zaidi duniani. (**Marca)**

### DE LIGT AFUATILIWA

KLABU ya Manchester United inamfuatilia kwa karibu beki wa Bayern Munich na Uholanzi, Matthijs de Ligt mwenye miaka 24. (**Sky Sports Germany**)

### TODIBO AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United pia inamtaka Jean-Clair Todibo mwenye umri wa miaka 24. (**Mail**)

### ZIRKZEE KWENYE RADA

MSHAMBULIAJI wa Bologna Mholanzi, Joshua Zirkzee mwenye Mika 23 pia yuko kwenye rada za Manchester United msimu huu wa majira ya joto, lakini wanaweza kukabiliwa na ushindani kutoka kwa AC Milan na Juventus. (**Telegraph**)

### YORO ATAKIWA EPL

LIVERPOOL na Manchester United zote zinamsaka beki wa kati wa Lille, Mfaransa Leny Yoro mwenye miaka 18, lakini Real Madrid pia wanamtaka. (**Athletic)**

### ABRAHAM AGOMBEWA

KLABU za Tottenham, Aston Villa na West Ham zinavutiwa na mshambuliaji wa Roma na England Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 26. (**Telegraph**)

### DURAN ANYATIWA VILLA

KLABU ya Aston Villa inahitaji pauni milioni 40 kumnunua mshambuliaji Jhon Duran, huku Chelsea wakiwa kwenye mazungumzo ya kumsajili mchezaji huyo mwenye miaka 20. (**Times**)

### MOURINHO AMTAKA HOJBJERG

KOCHA mpya wa Fenerbahce, Jose Mourinho anataka kumsajili kiungo wa kati wa Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg mwenye miaka, 28, kutoka Tottenham. (**Takvim**)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MAN UTD YAMALIZANA NA BRANTHWAITE

**MANCHESTER,** England

**Mashetani hao walikuwa wanawinda angalau beki mmoja baada ya kuondoka kwa....**

MANCHESTER United imefikia makubaliano ya kibinafsi na beki wa kati wa Everton, Jarrad Branthwaite, kwa mujibu wa ripoti.

**United wanawinda angalau beki mmoja mpya wa kati msimu huu wa majira ya joto baada ya kuondoka kwa Raphael Varane, huku kukiwa na maswali zaidi kuhusu mustakabali wa Harry Maguire, Victor Lindelof na Jonny Evans.**

Branthwaite mwenye miaka 21 alikuwa kwenye ubora msimu uliopita baada ya kufanya vyema katika mechi zake 41 kwenye michuano yote, gazeti la The Times limesema United wamefanya uamuzi wao wa kwanza kuhusu uhamisho wa majira ya kiangazi.

Maslahi binafsi yanaaminika kuwa yamekubaliwa na wawakilishi wa Branthwaite, ambao wanataka mkataba wa kulipwa mshahara wa kati ya pauni 150,000 na pauni 160,000 kwa wiki.

United lazima sasa wafanye mazungumzo ya ada ya uhamisho na Everton, ambao thamani ya Branthwaite wameiweka kuwa pauni milioni 70..

Iwapo wanataka kumpoteza Branthwaite, Everton wako tayari kudai ada kubwa, wakiamini kuwa beki huyo ni miongoni mwa vijana wenye vipaji maalum barani Ulaya.

United wanaripotiwa kufanya kazi na bajeti ya awali ya uhamisho ya pauni milioni 50 pekee, huku Sir Jim Ratcliffe akiipa changamoto klabu hiyo kuongeza fedha zaidi kupitia mauzo ya wachezaji.

## HABARI MICHEZO

# RONALDO: URENO INASTAHILI KUSHINDA EURO 2024



**BERLIN,** Ujerumani

CRISTIANO Ronaldo amesema kuwa kizazi cha sasa cha wachezaji wa Ureno kinastahili kushinda Ubingwa wa Euro 2024.

Nahodha wa Manchester United Bruno Fernandes, Vitinha wa PSG, na nyota wa Manchester City, Bernardo Silva na Rúben Dias ni miongoni mwa wachezaji wenye hadhi ya juu katika timu ya Ureno inayolenga kushinda taji hilo mwaka huu nchini Ujerumani.

Mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or alisema: "Ninaamini kwamba kizazi hiki kinastahili kushinda shindano la ukubwa huu. Nusu fainali? Natumaini tunaweza kwenda mbali zaidi.

"Lazima tuende hatua kwa hatua, tuishi kwa sasa, tuwe watulivu, tufanye kazi kama tulivyo hadi sasa, tuamini kwamba inawezekana. Tunajua ni mashindano mafupi, lakini timu iko tayari."

Ronaldo atashiriki kwa mara ya sita ya michuano hiyo Ujerumani, pamoja na wachezaji wengine wawili wa kikosi cha sasa, Pepê na Rui Patrício ambao walikuwa sehemu ya kikosi cha Ureno kilichoshinda Euro 2016.

"Ninafurahia mpira wa miguu, rekodi ni matokeo," alisema.

"Ni michuano yangu ya sita ya Ulaya, ni juu ya kufurahia kwa njia bora zaidi, kucheza vizuri na kuhakikisha timu inaweza kushinda."

Hii itakuwa michuano yake ya kwanza chini ya kocha Roberto Martinez, kocha wa zamani wa Ubelgiji.

Ureno itacheza na Jamhuri ya Czech katika mechi ya kwanza ya Kundi F Juni 18 kabla ya mechi dhidi ya Uturuki na Georgia.

Katika ushindi wa 3-0 wa kujiandaa kwa Ureno dhidi ya Jamhuri ya Ireland, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 39 alifunga mara mbili, na kuongeza rekodi yake ya mabao ya kimataifa kwa wanaume hadi kufikia 130.

# Kocha ammwagia sifa Toni Kroos Ujerumani ikiweka rekodi Euro



**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA Julian Nagelsmann amesema Toni Kroos alitoa mazungumzo "ya nguvu sana" kwa timu ya Ujerumani kabla ya wenyeji wa Euro 2024 kuweka rekodi ya ushindi wa 5-1 dhidi ya Scotland katika mchezo wa ufunguzi wa michuano hiyo mjini Munich.

Mabao kutoka kwa Florian Wirtz, Jamal Musiala, Kai Havertz, Niclas Füllkrug na Emre Can yaliwawezesha Wajerumani kupata ushindi mkubwa zaidi kwenye mchezo wa ufunguzi katika michuano ya Ulaya.

Scotland, walishindwa hata kupiga shuti lililolenga lango lakini walipata bao la kujifunga la Antonio Rüdiger.

Ushindi huo unaifanya timu ya Nagelsmann kuwa kinara wa Kundi A kabla ya mechi dhidi ya Hungary na Uswisi.

Lakini pamoja na Musiala na Wirtz, wote wenye umri wa miaka 21, wakiwa wamebeba presha ya timu changa kwenye michuano hiyo, kocha huyo wa Ujerumani alitoa pongezi kwa Kroos mwenye umri wa miaka 34, ambaye atastaafu mwisho wa mashindano hayo, kwa kusaidia kuwatuliza wachezaji kabla mchezo.

"Yeye ni muhimu sana, kama kila mtu mwingine," alisema Nagelsmann katika mkutano wake na waandishi wa habari.

"Timu ilikuwa na sauti kubwa kabla ya mchezo na alisema maneno machache ya utulivu ambayo yalikuwa na nguvu sana.

"Yeye ni sehemu ya kundi, lakini uzoefu wake ndio unamfanya awe tofauti, kwa rekodi yake wengine wangekuwa na matatizo ya kukubalika, lakini hana kiburi, ni muhimu sana kwa timu na ni mtulivu.

"Lakini licha ya mafanikio na hadhi yake yote, tunamwona kama sehemu ya kundi la wachezaji wetu."

# Walker nahodha msaidizi England

**BLANKENHIN,** Ujerumani

KYLE Walker amechaguliwa kuwa nahodha msaidizi mpya wa England kwenye michuano ya Ulaya nchini Ujerumani, vyanzo vimeiambia ESPN.

Mchezaji huyo mwenye miaka 34 alifahamishwa kuhusu uamuzi wa Gareth Southgate mapema mwezi huu na anachukua nafasi muhimu ya uongozi katika kikosi ambacho kimepata mabadiliko makubwa tangu michuano yao wa mwisho, Kombe la Dunia la 2022.

Ni nusu tu ya kikosi cha wachezaji 26 waliosafiri hadi Qatar ndio waliochaguliwa kwa Euro 2024 huku kocha Southgate akirekebisha kundi lake la uongozi.

Walker anachukua nafasi ya Jordan Henderson, ambaye ameachwa nje ya kikosi wakati huu baada ya kushindwa kuthibitisha ukali wake baada ya kurejea hivi karibuni kutoka Ajax akiwa na jeraha la misuli ya paja.

Beki huyo wa Manchester City ndiye mchezaji wa pili katika kikosi hicho aliyecheza mechi nyingi zaidi katika kikosi hicho akiwa amecheza mechi yake ya 83 katika mechi ya kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Iceland Ijumaa iliyopita. Nahodha Harry Kane anaongoza akiwa na mechi 91.

Huku Harry Maguire na Raheem Sterling wakiwa miongoni mwa walioachwa pia, Kieran Trippier na Declan Rice ni sehemu ya kundi jipya la uongozi wa Southgate waliopewa jukumu la kusaidia wachezaji 12 ambao hawajawahi kushiriki michuano mikubwa kabla ya kutua Euro 2024.

Trippier alikuwa nahodha wa England katika mchezo wao wa kwanza wa kujiandaa dhidi ya Bosnia huku Rice akitangazwa kuwa nahodha Machi katika mechi yake ya 50 ya kimataifa.



## HABARI MICHEZO

# NKANE AWINDWA NA MASHUJAA

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Mashujaa FC inamuwinda winga wa Yanga, Denis Nkane, ambaye wanaona anaweza kukiongeza nguvu kikosi chao kwa ajili ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa tayari wameanza mazungumzo na mchezaji huyo ambaye amekuwa hapati nafasi ya kucheza kwenye kikosi cha Mabingwa wa Tanzania Bara.

"Tunaongea na Nkane, siyo mchezaji mbaya, ana kipaji, ni winga mzuri, ana mbio, siyo mvivu, ni kwa vile Yanga kuna wachezaji wengi wenye ubora wa hali ya juu na yeye hachezi mara kwa mara, kama anakuja kwetu ambako atacheza mechi nyingi atarudi kwenye ubora wa hali ya juu, inawezekana kuliko alivyokuwa mwanzo wakati anatoka Biashara United kujiunga na Yanga," alisema mtoa taarifa ndani ya klabu hiyo.




Mchezaji huyo anayecheza winga ya kushoto, alijiunga na Yanga, 2022, akitokea klabu Biashara United, lakini kipindi chote hicho amekuwa na changamoto ya kupata namba kwenye kikosi cha kwanza, na kuna wakati akaandamwa na majeraha.

Mtoa taarifa huyo alisema maandalizi yote ya msimu ujao yanaelekea kukamilika likiwemo suala la usajili na Juni 28, wanatarajia kwenda Zanzibar kwa ajili ya kupiga kambi kwa ajili ya maandalizi ya Ligi Kuu msimu wa 2024/25.

"Tarehe 28 mwezi huu tunategemea kuanza maandalizi ya msimu ujao 'pre-season', tutafranyia maandalizi yetu Zanzibar.

Kuhusu maboresho, mwalimu ameshatoa ripoti yake, tumeifanyia kazi, tumeongeza baadhi ya wachezaji, tutawatangaza rasmi majina yao tutakapokuwa tayari kufanya hivyo. Kwa kikosi cha msimu ujao malengo yetu ni nafasi nne za juu," alisema.

Mashujaa, yenye maskani yake Mkoani Kigoma, ilimaliza ligi msimu uliomalizika ikiwa kwenye nafasi ya nane ikicheza mechi 30, imeshinda mechi tisa, sare nane na ikapoteza mechi 13 na kukusanya pointi 35.

## KIKAPU




Wachezaji wa timu ya mpira wa Kikapu ya Vijana, wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# 'Kuotea' kwa vunja mechi ya fainali FA Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

MCHEZO wa Fainali ya kombe la FA Zanzibar umelazimika kuvunjika katika muda wa ziada baada yadakika 90 baada ya mwamuzi kukataa goli la pili la JKU.

Mwamuzi wa mchezo huo, Mohamed Amour alilikataa bao hilo kwa kuwa mfungaji alikuwa ameotea.

Mchezo huo wa fainali ulikuwa unachezwa kwenye uwanja wa Gombani, Pemba kati ya JKu dhidi ya wenyeji wao mChipukizi FC.

Mchezo huo ulilazimika kuongezwa dakika 30 za ziada baada ya dakika 90 kukamilika kwa timu zote kufungana bao 1-1.

Bingwa wa Michuano hiyo ataiwakikisha Zanzibar katika michuano ya Kombe la Shirikisho Barani Africa.

Akizungumza na gazeti hili Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya Shirikisho la Soka visiwani hapa (ZFF), Suleiman Haji 'Kibabu', alisema sababu kubwa iliyopelekea kuvunjika mchezo huo ni baada ya kukataliwa goli la JKU katika dakika hizo za ziada na jambo lililopelekea kutokera vurugu zilisababisha mchezo huo kuvunjika.

Alisema baada ya kutokea vurugu hizo ambazo zilifanikiwa kutulizwa na maafisa usalama wa mchezo huo lakini cha kushangaza baada ya utulivu Mwamuzi aliamua kuuvunja mchezo huo.

"Bado hakukuwa na sababu ya msingi kwa maamuzi aliyoyachukua mwamuzi huyu pasipo kuwashirikisha waamuzi wenzake, licha ya kutokea vurugu lakini zilifanikiwa kutulizwa"alisema.

Hata hivyo alisema tayari washakutana na kufanya kikao juu ya mchezo huo na watatoa maamuzi kwa mujibu wa kanuni ya mashindano ya masimu wa 2023/2024.

# Joshua Mutale apewa miaka mitatu Simba

INATOKA UK. 24

mchezo wa raundi ya kwanza, Ligi ya Mabingwa Afrika, Septemba 16 mwaka jana nchini Zambia, timu hizo zikitoka sare ya mabao 2-2, na alikuwa mwiba kwa mara nyingine katika mechi ya marudiano, Oktoba Mosi, mwaka jana, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1 na Simba kutinga hatua ya makndi kwa faida ya mabao mengi ya ugenini.

Baadhi ya wachezaji wanaotajwa kuwa huwenda wakatua Msimbazi ni winga mwingine anayeichezea klabu ya AS Vita ya Jamhuri ya Kidemkorasi ya Congo, Elie Mpanzu, mshambuliaji Derrick Fordjour kutoka Medeama ya Ghana.

Pia imetajwa kumuwinda mshambuliaji Ricky Banda, raia wa Zambia anayeichezea Red Arrows ya nchini humo, mlinzi wa kati wa Mamelodi raia wa Kenya, Brian Mandela Onyango, mshambuliaji Agostinho Mabululu raia wa Angola anayechezea klabu ya Al Ittihad ya Misri, na kiungo mkabaji Ibrahim Gadiaga wa FC Nouadhibou ya Mauritania.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo Ahmed Ally, ametangaza rasmi kuwa kuanzia kesho Jumatatu wataanza kutangaza wachezaji walioachwa, wakifuatiwa na wale walioongeza mikataba, kabla ya kutangaza wapya waliosajiliwa.

Amesema wachezaji, watakaoachwa ni wale ambao viwango vyao haviridhishi, umri mkubwa, majeraha sugu na utovu wa nidhamu.

"Kikubwa ambacho watu wanataka kusikia ni nani anaondoka ndani ya klabu na nani anaingia, taarifa zote muda si mrefu zitaanza kutoka, kuanzia Jumatatu tutaanza kutoa taarifa ya wale wanaoondoka, baadaye tukimaliza, tutakuja na wale ambao wameongeza au tumewaongezea mikataba, mwisho kabisa tutaanza sasa taarifa rasmi za usajili," alisema Meneja Habari huyo.

Alisema imewalazimu safari hii kufanya upembuzi yakinifu, tathimini na umakini wa hali ya juu kumuangalia mchezaji mmoja mmoja na mchango wake katika timu.



"Kila mmoja anafahamu tumefanya vibaya msimu uliopita kwa hiyo ni lazima kwanza ufanyike upembuzi yakinifu, kwa sasa tumeshamaliza kupitia ripoti ya walimu wote, waliopita na waliopo, kitu gani wamependekeza na nini kifanyike kwa ajili ya msimu ujao, kilichobaki ni utekelezaji wa hizo ripoti," alisema Ahmed.

# Michezo

Jumapili Juni 16, 2024
Nipashe



## Man Utd yamalizana na Branthwaite



Mshambuliaji wa timu ya taifa ya Ujerumani, Jamal Musiala (kulia) akipiga mpira mbele ya beki wa Scotland kwenye mchezo wa ufunguzi wa fainali za Ulaya 'Euro 2024' juzi usiku, Ujerumani ambao ndio wenyeji wa michuano hiyo walishinda mabao 5-1. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA KUPIGA KAMBI ULAYA, KUFANYA ZIARA KENYA, SAUZI

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Yapata mualiko kutoka Mamelod Soundown na wataenda Afrika Kusini baada ya...

KIKOSI cha Yanga kinatarajiwa kufanya ziara nchini Kenya na Afrika Kusini, huku safari hii kikiweka kambi yake barani Ulaya, tayari kwa msimu mpya wa mashindano msimu ujao.

**Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Ofisa Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema safari hii kambi yao haitokuwa Kigamboni kama ilivyo kawaida, badala yake wataelekea barani Ulaya, tayari kwa maandalizi.**

"Napenda niwafahamishe wanachama na mashabiki wa Yanga kuwa tunatarajia kufanya ziara nchini Afrika Kusini kwa mwaliko wa klabu ya Mamelodi Sundowns, tuna mialiko pia nchini Kenya kwenye ufunguzi wa uwanja, na safari hii tutakwenda kuweka kambi yetu Ulaya, ni nchi gani? tutakuja kuwajulisha, ila kambi yetu msimu wa maandalizi haitakuwa Kigamboni, badala yake wachezaji watakutana Kigamboni baada ya mapumziko yao na baadae kuanza safari ya kwenda Ulaya," alisema Kamwe.

Akizungumzia usajili alisema watafanya usajili makini na kwa bahati nzuri, dirisha la usajili limefunguliwa kipindi cha kuanza mwaka wa fedha kwa klabu hiyo.

"Usajili umefunguliwa na mwaka wetu wa fedha wa klabu unaanza Julai Mosi, uliomalizika hatukuwa na majina makubwa, ila tulikuwa na wachezaji bora kama Pacome Zouzoua, Maxi Nzengeli na Yao Koassi, uwezo wao uliwashtua Watanzania. sisi hatuendeshwi na propaganda au mitandao ya kijamii, nimeuchungulia usajili wetu kidogo nimeona majina ya wachezaji wasio na majina makubwa lakini ni bora, pia wenye majina makubwa msimu ujao wapo tutakuwa nao," alisema Ofisa Habari huyo.

Yanga pamoja na kutwaa Ubingwa wa Tanzania Bara mara ya tatu msimu huu, lakini imekuwa na kiwango bora na msimu wenye mafanikio, ambapo mbali na ubingwa huo, imetwaa Kombe la FA, pamoja na kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ikitolewa kwa mbinde na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.

Kwa mujibu wa viongozi wa klabu hiyo, wanataka kutengeneza kikosi bora zaidi kuliko msimu uliopita ili kuvuka mafanikio waliyoyapata msimu uliopita.

# Joshua Mutale apewa miaka mitatu Simba

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU moja baada ya dirisha la usajili kufunguliwa, hatimaye klabu ya Simba imefanikisha usajili wa winga machachari wa Power Dyamos ya Zambia, Joshua Mutale kwa kumsainisha mkataba wa miaka mitatu.

Habari za uhakika kutoka ndani ya klabu hiyo, zinasema kuwa mchezaji huyo, mwenye uwezo wa kucheza winga zote mbili, pamoja na namba 10, alikamilisha kutia saini jana jioni nchini Zambia, ambapo mkataba wake utamalizika Juni 2027.

Nipashe inafahamu siku tatu zilizopita mmoja wa watu waliopewa kazi ya kufanya usajili na Mwekezaji, Rais wa Klabu hiyo na Mwenyekiti wa Bodi, Mohamed Dewji alikwenda Zambia kukamilisha dili hilo.

"Nilikwambia kuwa jamaa aliyekuwa Zambia yuko katika hatua za mwisho, sasa ni rasmi, Mutale amesaini kuichezea Simba leo jioni (juzi), safari hii watu hawataki mchezo, hakuna mkataba wa miaka miwili, tukiwa na uhakika kuwa mchezaji huyo ni mzuri, umri mdogo na anaweza kutupa mafanikio, tunampa miaka mitatu," alisema kiongozi mmoja ndani ya klabu hiyo.

Inaelezwa kuwa mchezaji huyo anakuja kuchukua nafasi ya Luis Miquissone ambaye ameshindwa kuonyesha makali yake tangu aliporejea kutoka Al Ahly ya Misri mwanzoni mwa msimu huu, huku tetesi zikisema tayari UD Songo ya nchini kwao, Msumbiji imeonyesha nia ya kutaka kumrudisha nyumbani nyota huyo.

Mutale, raia wa Zambia, aliwachachafya mabeki wa Simba, hasa Shomari Kapombe, katika mechi ya tamasha la Simba Day iliyochezwa Agosti 6 kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa, Simba ikishinda mabao 2-0, lakini pia aliwafanya anavyotaka katika

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >